

MSIOGOPE, NI MIMI



...sana Ndugu Herman. Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa mengine kuwa hapa usiku wa leo, katika utumishi wa Bwana, kujaribu kufanya tuwezavyo kuwasaidia watu kumjua Bwana Yesu vizuri zaidi. Tumekuwa na wakati mzuri sana juma hili. Kama kuna wageni usiku wa leo, tuna uamsho tu wa mtindo wa kale. Ninapowaona watu wakishuka kwenye marefu ya kanisa hapa kumkubali Kristo kama Mwokozi wao, wakiingia kutafuta, na kumwomba Mungu waweze kutembea kwa kina zaidi pamoja Naye, na kumpokea Roho Mtakatifu, hiyo inamaanisha kwamba kuna uamsho unaoibuka. Kwa hiyo tunashukuru, tunashukuru sana, sana kwa ajili ya jambo hilo. Nami ninatumaini ya kwamba Bwana Yesu atatubariki usiku wa leo, sana.

² Na, sasa, ninawatakeni mkumbuke kiamshakinywa cha kesho asubuhi. Nafikiri kimefutwa kisiwe ni kwa ajili ya wahudumu na wake zao tu, bali ni “yeyote atakaye,” na mahali fulani hapa uwanjani, shuleni, ambapo hicho kiamshakinywa kitakuwako. Ndipo mara baada ya kiamshakinywa nataka ku—kuzungumza, kulihutubia ku—kundi lililoko kule...juu ya ujumbe wa kiinjalisti. Na bila shaka ningefurahi kama mngeweza kupata wakati katika ratiba yenu, kwa kuwa ni Jumamosi, kama mngeweza tu kuja kwa dakika chache na kula kiamshakinywa pamoja nasi, na kusikiliza ujumbe.

³ Halafu—halafu Jumamosi usiku, kesho usiku, kwenye wakati wa kawaida, saa moja na nusu, nafikiri, ni mwanzo wa ibada ya kawaida tena, kesho usiku. Halafu Jumapili alasiri, saa nane, tunatarajia mkutano mwingine mkubwa wa kuwaombea wagonjwa, Jumapili alasiri, kuondoka, wakati, kabla hatujaondoka mjini. Asanteni kwa mwaliko wenu kurudi, nami ninatumaini ya kwamba yakiwa ni mapenzi ya Bwana, nitarudi pamoja nanyi tena, wakati mwingine; umekuwa ni wakati mzuri sana.

⁴ Sasa, sitaki kuchukua muda mwingi sana, usiku wa leo, husema hivyo kila usiku, tunaondoka yapata saa nne, ama saa nne na nusu, ama mahali fulani namna hiyo, bali ninyi ni kusanyiko zuri sana la kuzungumzia. Sasa, nataka, kwa sababu usiku wa leo tutawaombea wagonjwa...Hakika kila usiku tumewaombea wagonjwa, wazieni, kila usiku. Sasa, ili tupate ufahamu mzuri, dhahiri katika kila mtu, nami ni...Nitawaomba iwapo mtakuwa na kicho vivyo hivyo, na mnisikilize kwa makini, kwa sababu wapo watu walioketi hapa, na huko nje kwenye kusanyiko, na wasipopata usaidizi kutoka kwa Mungu, watatuacha mara moja.

⁵ Sasa, vipi kama huyu alikuwa ni mama yako aliye kwenye machela hii? Vipi kama huyu alikuwa ni baba yako ameketi kwenye kiti hiki cha magurudumu? Vipi kama huyo alikuwa ni mtoto wako amelala hapo? Unaona, huenda usiamini katika uponyaji wa Kiungu, bali hujawahi kuwa mgonjwa vya kutosha bado, hujawahi kuwa na daktari akitikisa kichwa chake, na kusema, “Inahitaji Mungu kutokea hapo, nimefanya yote niwezayo kufanya,” utaamini katika uponyaji wa Kiungu basi.

⁶ Kwa hiyo, kumbukeni ni jambo lililoandikwa katika Maandiko, kama ungemkataa Yeye katika siku za afya yako namna hii basi msiba wako ujapo Yeye alisema, “Nitakucheka tu.” Kwa hiyo ni bora zaidi kumjua sasa, wakati ukiwa na afya nzuri, na mwenye akili timamu, na unaweza kumwendea, na kumkubali, na kuliadini Neno Lake, na kujielezea Kwake, ni bora zaidi kumjua Yeye sasa, kusudi saa ya shida itakapokuja, Yeye ni msaada upatikanao wakati wa shida.

⁷ Sasa, na ijulikane kwa kila mtu, ya kwamba siamini ya kwamba kuna kitu kama mwanadamu kuwa mponyaji wa Kiungu. Awe ni daktari, ama kama ni mtaalamu wa magonjwa ya akili, chochote alichu, hakuna waponyaji wa Kiungu, kuna Mponyaji mmoja tu, na huyo ni Mungu.

⁸ Sasa, tuna madaktari, na taasisi za matibabu, na wanasayansi wa kufanya utafiti wa dawa, na ambao tunashukuru, na kama Wakristo hatupaswi kuacha siku moja ipite bila kuomba usaidizi wa watu hao ambao wanajaribu kunini, katika utafiti kupata kitu cha kusaidia kuwaondolea mateso. Nafikiri ni jambo halisi, tendo halisi la Kikristo, kwa wanaume na wanawake kuwaomba watu wapate *kitu fulani* cha kutusaidia. Kwa sababu, vipi kama wewe ndiwe uliyekuwa mgonjwa? Unaona? Ungetaka chochote ambacho kingeweza kukusaidia. Vema, basi mtu anapofikia mahali ambapo wana . . . ambapo daktari hawezi kukufanyia cha zaidi, basi nafikiri tuna haki ya kumwita Mungu, sisi tunaomwamini Mungu.

⁹ Sasa, haikanushiki katika Maandiko kuhusu Yesu Kristo na wale mitume wa mwanzoni, kweli, kwa imani, waliwaponya wagonjwa. Yesu alidai ya kwamba Yeye kamwe hakuwaponya wagonjwa, alisema, “Ni Baba Yangu aishiye ndani Yangu, Yeye huponya, nami hufanya tu kulingana na vile Yeye anavyonionyesha kwa ono.” Sasa, mwanafunzi yeyote wa Biblia anajua hiyo ni kweli, Yohana Mtakatifu 5:19. Yesu kamwe hakufanya mwujiza mmoja maishani Mwake bila kwanza Mungu Baba kumwonyesha ono la kuufanya, la sivyo Yeye alisema jambo baya katika Biblia, kwa kuwa Yeye alisema, “Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, bali lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.”

¹⁰ Sasa, uponyaji wa Kiungu haujawekwa juu ya mhemko

fulani, haujajengwa juu ya kuwekewa mikono, au hisia fulani ya kiajabuajabu, ama mhemko, imewekwa msingi juu ya imani katika kazi uliyofanyiwa na Yesu Kristo pale Kalvari; ni kazi iliyomalizika. Na kila mtu hapa, usiku wa leo, ambaye ni mgonjwa na anateseka, kulingana na Mungu, tayari umeponywa. Mnaona? Na kila mwenye dhambi hapa tayari ameokolewa, kwa kuwa ilimalizika pale Kalvari.

¹¹ Na sasa, kwa washauri na waalimu wa hizi shule, kama lile agano la kale, ule upatanisho wa kale ulijumuisha uponyaji, na huu ni upatanisho bora kuliko ule wa kale ulivyokuwa, ni zaidi sana vipi huu ulivyo na uponyaji ndani yake? Mnaona?

¹² Biblia ilisema, katika Isaya, ya kwamba alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa. Sasa, mtu fulani alijaribu kuzungumza, na kusema hilo lilitimizwa katika Mathayo 12 aliposema alijitwika udhaifu wetu, Naye akauponya, ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya, “Yeye aliuchukua udhaifu wetu.” Hiyo ilikuwa ni mwaka mmoja na miezi sita kabla ule upatanisho kufanywa. Basi kama hiyo ni kweli, ambapo wengi wanajaribu kubishana dhidi ya uponyaji wa Kiungu, basi ule upatanisho ulikuwa na nguvu zaidi kabla haujaanza kutumika, kuliko ulivyokuwa baada ya kuanza kutumika. Kwa hiyo wewe . . .

¹³ Nami ninaweza kumwonyesha mtu yeyote, ama, msomaji yeyote wa Biblia, ambapo Kristo alilipa Kanisa Lake, kama linaitwa Methodist, Baptisti, Presbiteri, Katoliki, Pentekoste, chochote kile, aliwapa nguvu za kuwaponya wagonjwa. Sasa, ninamwomba mtu yeyote, mwanafunzi yeyote, mwanafunzi yeyote wa Biblia, ama mwanahistoria, kuniletea kipande kimoja cha Maandiko ambapo Yesu aliondoa nguvu hizo kutoka kwa Kanisa, na kuwaambia hawakuwa nazo tena. Kamwe hakuondoa hayo mamlaka kutoka kwa Kanisa, Kanisa linaogopa kutekeleza ama kutenda yale Kristo aliyowaambia wafanye.

¹⁴ Sasa kwa mkosoaji, miaka michache iliyopita ungeweza kutoa matamshi, lakini sasa tuna makumi ya maelfu ya taarifa zilizoidhinishwa na madaktari, zahanati, hospitali, kila mahali kote ulimwenguni, za miujiza ya ajabu kabisa ya vipofu, viziwi, bubu, waliofufuliwa kutoka kwa wafu, wakati daktari aliwatangaza kwamba wamekufa, taarifa zilizoidhinishwa. Kwa hiyo kuna . . . Vinywa vya—vyao . . . kinywa cha asiyeamini kimenyamazishwa. Mnaona? Hamsikii mengi zaidi yake, sivyo? Hakuna la kusemwa.

¹⁵ Sasa, hilo si la Wapentekoste tu, hilo si la kundi fulani tu, ama mtu fulani, ama mwi—mwinjilisti wa kupita, kama mimi mwenyewe, ama Bw. Roberts, ama mtu mwingine, hilo ni kwa kila mwaminio, si kwa mchungaji tu, bali kwa walei, kwa mwanamume yeyote ama mwanamke aliyezaliwa na Roho wa

Mungu, aliye na imani katika uponyaji, ana haki ya kuwaombea wagonjwa pamoja na matokeo yale yale ambayo mtu mwingine yeyote angepata.

¹⁶ Si...Mimi si mmoja wa wanaoamini katika Unikolai, kuchukua ninii yote...“kuwashinda walei na kuyaweka yote katika mchungaji,” iko katika walei. Roho Mtakatifu kamwe hambatizi tu mchungaji, Yeye huwabatiza walei, pia, yote yako katika walei, na mchungaji ni mmoja wetu tu. Linamaanisha, “mchungu kondoo,” *mchungaji*, ambalo linamaanisha “mlishaji wa kundi.” Roho Mtakatifu humtoa mwangalizi kuliangalia, na kuliongoza.

¹⁷ Sasa, kumbukeni, kama Yesu wa Nazareti alisimama hapa kwenye jukwaa hili usiku wa leo, amevaa suti hii aliyonipa, na yeyote wenu ninyi watu wa thamani hapa angemjia, na kumwomba akuponye, asingeweza kufanya hivyo. Sasa, hilo linaonekana ni la kigeni, bali Yeye asingeweza, kwa sababu tayari amelifanya, umekombolewa. Unaona? Angesema, “Mimi...Kama unaamini, tayari umeponywa.”

¹⁸ Mtu fulani alisema, “Niliponywa...Niliokoka juma lililopita, Ndugu Branham.” Samahani. “La, niliokoka miaka kumi iliyopita.” La, uliokoka miaka elfu moja mia tisa iliyopita, wakati Kristo alipokufa, Yeye alilitatua swali la dhambi.

¹⁹ Basi unawezaje kamwe kuhubiri wokovu wa nafsi bila kuhubiri uponyaji wa Kiungu? Kwa sababu ugonjwa huo ni matokeo ya dhambi, kabla hatujawa na dhambi hatukuwa na ugonjwa, nao ugonjwa uliletwa na dhambi, labda si jambo ulilofanya, ni kitu ulichorithi.

²⁰ Leo katika mahojiano ya faraghani (Ambapo, hapo ndipo mahali unapapaswa kumwona Roho Mtakatifu.), kuna wanaume na wanawake wanaoketi hapa usiku wa leo, ambao hata Roho Mtakatifu anarudi nyuma kabisa, leo hii, kufikia vizazi vitatu, na kuwashusha hao watu, na kuwaambia jina lao, na yale waliyofanya, na yote kuyahusu, na ni kwa nini kitu hiki kilikuwa juu ya mtu huyu, na kukiondoa kwao, na kuwaponya, wakisimama moja kwa moja chumbani. Anawaambia nyanya yao, babu yao, walikuwa nani, walitoka wapi, waliyofanya. Kizazi cha tatu wasingeweza kuwazia, lakini kizazi kilichofuata kililiweka wazi, na kizazi kilichofuata, halafu wao, kwao, bila shaka walijua. Mnaona? Ye—Yeye anajua mambo yote.

²¹ Sasa, hilo halikumponya huyo mtu, bali liliwainua kufikia mahali ambapo walikuwa na imani ya kuponywa, hiyo ndiyo sababu tuna matendo. Kwa nini tunabatiza? Maji hayatakuokoa, bali ni kutii tendo fulani. Kula ushirika hakutakuokoa, bali ni kufuata amri. Unaninii tu...Kupigapiga madhabahuni hakutakuponya, kupigapiga madhabahuni hakutakuokoa, ungeweza kupigapiga madhabahuni mpaka ukaishiwa tu na pumzi na—na kufia pale, ungali ungekuwa hujaokoka, mpaka

utakapokubali na kuamini ya kwamba Yesu alikufa badala yako, nawe umkubali kama Mwokozi wako binafsi. Kila mhadumu hapa ndani angeweza kuweka mikono juu ya kila mgonjwa hapa ndani, na kuomba tangu sasa, mpaka kesho kutwa usiku, kamwe kusingetukia lolote, mpaka utakapokubali yale Yesu aliyokufanyia. Kwa hiyo, basi haliko juu ya wahudumu, katika mmoja kwa mwingine, bali liko katika imani yetu binafsi katika kazi iliyomalizika ambayo Kristo alitufanyia pale Kalvari.

²² Sasa, kwanza . . . Sasa, watu wengi wameniita mponyaji wa Kiungu, na watu wengine wameniita, hilo, ndugu, hakika mnajua vizuri zaidi ya hivyo. Kama unaamini . . . Kama mchungaji wako akihubiri wokovu, nawe uokoje, kwa sababu wokovu uko katika Biblia, basi unapookoka chini ya mahubiri yake, je, hilo linamfanya kuwa mwokozi wa Kiungu? Si zaidi ya vile ingemfanya mtu mwingine yeyote anayehubiri uponyaji kuwa mponyaji wa Kiungu, kwa sababu sisi tunaninii tu, tunakiri yale Yesu aliyosema.

²³ Naye Yesu ndiye Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, ameketi mkono wa kuume wa Mungu kutuombea tunapoungama. Ninajua King James inasema *kuungama*, na *kukiri* ni neno lile lile. Lakini *kukiri*, Naye hawezi kukufanyia lolote, mpaka kwanza uamini, ulikubali, na kukiri kwamba ni kweli, basi Yeye ndiye Kuhani Mkuu kufanya maombezi juu ya yale unayokiri kwamba Yeye amekufanyia. Hilo ni dhahiri tu kama ni—ninavyojua Injili. Hiyo ni, kwa kweli hiyo—hiyo tu ndiyo mimi. . . hiyo ndiyo Injili pekee iliyopo, ndiyo hiyo. Sasa, kila mtu anayeelewa hilo. . .

²⁴ Pia jambo lingine ninalotaka kusema, kabla sijauliza, ama, kusema tena, sasa, kwanza, imani chanzo chake ni nini? “Kusikia,” na kusikia “Neno la Mungu.” Sasa, hilo linapaswa kutosha, lingetosha kwangu mimi, lingetosha kwako, wasipoamini neno lako, achana nao. Lakini sivyo ilivyo kwa Bwana wetu Yesu. La, sivyo ilivyo. Yeye hutuma karama Kanisani.

²⁵ Hakuna mtu awezaye kukana ya kwamba karama haziko katika Kanisa la Mungu aliye hai. Wakorintho wa Kwanza 12 ilisema kuna karama tisa za kiroho katika kila mwili, na pia kuna ofisi tano za kiroho Kanisani, kwanza, kuna mitume, ama wamishenari, yote mawili yanamaanisha, hilo neno linamaanisha “mtu aliyetumwa.” Mitume, manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti, wote hao ni karama zilizoamriwa na Mungu kwa Kanisa. Wachungaji, wainjilisti, manabii, na wamishenari, ama mitume, Kanisani, hao wanatumwa huko, halafu karama tisa za kiroho zinawekwa katika kila shirika la mahali hapo.

²⁶ Basi ni kwa nini baadhi yenu watu, kanisa kuu kama kanisa la Presbiteri, ninayo folda yao, kasema, “Kwa muda

mrefu kanisa la Presbiteri limesahau kanuni za Kanisa la mwanzoni. Hatuna budi kurudi kwenye wanenaji wa lugha wa kanisa la Kipresbiteri, wafasiri wa lugha, karama za uponyaji, na ishara za Kanisa la mwanzoni lazima tena ziambatane na kanisa—ziambatane na kanisa, la sivyo kamwe hatutaendelea mbele zaidi.” Mungu ambariki mtu aliyeandika hayo. Hatuna budi kurudi kwenye ule mwanzo wa asili, tuliuundia tu madhehebu, na kufanya mafundisho ya sharti ya kujibunia, mpaka tukawafanya maskini hao watu wasijue la kuamini, ni tamasha la kusikitisha.

²⁷ Sasa, kumbukeni ya kwamba kile Kristo alichokuwa jana, ndicho alichio leo. Na mtu yeyote anajua, anayesoma Biblia, ya kwamba ishara Yake ambayo aliwathibitishia watu ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. . . Ni wangapi wanaojua ishara Yake ya Kimasihi ilikuwa nini, baada ya mafundisho ya juma hili? Inua mkono wako. Ni wangapi walio hapa kwa mara yenu ya kwanza basi? Loo, wengi. Jinsi alivyothibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi ni kwa sababu alikuwa ni Nabii, kwa kuwa Musa alisema ya kwamba angekuwa ni Nabii *huyu*.

²⁸ Sasa, nitazungumza, na mara moja, upesi niwezavyo, tutaingia basi kuwaombea wagonjwa. Sasa, kumbukeni, hayatakuwa tu ni maombi yangu, maombi *yenu*. Na tafadhalini, marafiki zangu ambao mmekuja hapa wagonjwa na wanaoteseka, hali mbaya sana, sana, mmeketi, baadhi yenu, kwenye viti vya magurudumu, baadhi yenu ni mahututi, nadhani, wengine wameketi hapo kwenye kusanyiko, bila nafasi ya kuishi nje ya Mungu, kumbukeni tu, yale ninayosema hapa, sina budi kukutana nanyi pamoja na ujumbe huo kwenye Siku ya Hukumu na kutoa hesabu kwa ajili yake.

²⁹ Ingenifaa nini kuwa hapa, mbali na familia yangu na wapendwa wangu? Ni—ningekuwa nikifanya nini hapa? Sichukui pesa, sio umaarufu, ni. . . Sininii. . . Ninajiepusha na jambo hilo, mnajua hilo. Kwa hiyo ni—ni ya nini? Ni kwa sababu kwamba Mungu aliniambia, alinituma, na kunionyesha katika Maandiko, na kulithibitisha kwa Malaika wa Bwana, kwamba nilizaliwa kusudi niwaombee wagonjwa. Na kwa sababu kwamba ninampenda Mungu, na kuwapenda watoto Wake, hiyo ndiyo sababu niko hapa usiku wa leo. Kweli kabisa.

³⁰ Sasa, kwenye ile Hukumu sote tutakutana na jambo hilo. Labda kuna watu elfu moja mia tano humu ndani usiku wa leo, nakisia, wengi hivyo. (Samahani?) Mimi—mimi ni duni sana kwa makadirio, anasema kuna karibu elfu moja mia tisa. A—a—afadhali niifanye ndogo, kuna hesabu nyingi sana za kiinjilisti zinazojaribu kuufanya umati kuwa mkubwa kuliko vile ulivyo. Nimehubiri mbele ya laki tano kwa wakati mmoja huko Bombay, India. Na huko Durban, Afrika Kusini, ilijadiliwa ambapo kulikuwa na watu mia moja na hamsini elfu, mia mbili. Watu elfu mia moja na hamsini, mia mbili si kitu katika nchi hizo,

katika Thailandi na mahali kama hapo ambapo wewe...kweli watu wanajitokeza, nawe unawaona kwa makumi ya maelfu na maelfu.

³¹ Huo, haumaanishi, umati wa watu haumaanishi chochote, cha muhimu ni ile imani iliyo ndani ya mtu binafsi. Mnaona? Yesu asingeweza kamwe kufanya kusanyiko la mmoja wa—wa wale makuhani, ama Kayafa, ama baadhi ya watu hao, wala yeyote wetu katika jamii ya kidini asingeweza kufanya mkutano mkubwa kuliko kanisa Katoliki, mnajua hilo. Lakini si katika...Tunatilia mkazo sana ni watu wangapi, na kujaribu kuinua kitu fulani, usiinue chochote, ku—kuwa tu mkweli juu yake, sema ukweli, ndipo sikuzote uko sahihi.

³² Na wakati unapoanza kuzungumza juu ya uponyaji, usijaribu kusema, “Nina kitu *fulani* mkononi mwangu, nakihisi?” Vema, huenda ukauhisi mkono wako, lakini uponyaji hauko mkononi mwako, uko katika Kalvari, ni katika imani yako, ambapo ilimalizikia Kalvari. Basi hebu watu...Ambao ni...Na iwapo wewe ni mwenye dhambi, tubu, mwambie Mungu ya kwamba unasikitika wewe ni mwenye dhambi, nawe ni mgonjwa (Labda, wakati mwingine ilimlazimu kukulaza chali, kusudi akufanye utazame *juu*, unaona.), na kisha ujiweke sawa na Mungu, ndipo basi kila kitu kitakuwa sawa, u mwepesi zaidi wa kuponywa kama utafanya hivyo.

³³ Sasa, ninajua kuna joto, nami nitajaribu kufupisha tu niwezavyo, ili tuweze kuwaombea wagonjwa. Sasa, ninyi watu wote mnaofahamu ya kwamba imani *yenu* katika Yesu Kristo ndiyo inayowaponya, semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Imeeleweka.

³⁴ Sasa, kuna karama katika Biblia, nazo karama hizo, zinafanya nini? Zinatangaza tu Uwepo wa Yule aliyeifanya hiyo karama. Sasa, kama Yesu alisimama hapa usiku wa leo, Mwenyewe, jukwaani, nawe ulijua ya kwamba—ya kwamba, Yeye angeshuka kutoka Mbinguni, nawe ulijua ilikuwa ni Yeye, Naye akasimama hapa, je, ingeinua imani yako? Hakika, ingeinua. Vema, Yeye *yupo* hapa.

³⁵ Unasema, “Ninajuaje Yeye yuko?” Vema, basi, kama Yeye akifanya jambo lile lile hapa ndani yetu...Sasa, Yeye hana mikono yoyote. Ni wangapi wanaojua hilo? La. Yeye...Mikono Yake, mikono yako ni mikono Yake. Sisi, Yeye ni Mzabibu, sisi ni matawi, nao Mzabibu hauzai tunda, tawi huzaa. Lakini kama tawi limetiwa nguvu kwa Uhai wa huo Mzabibu, litafanya mambo yale yale aliyofanya Yeye, ndipo utajua ni Yeye.

³⁶ Yeye alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena,” (bila shaka, neno hapo, *kosmos*, ambalo linamaanisha “utaratibu wa ulimwengu,”) “bali ninyi mtaniona Mimi,” huyo ni mwaminio, “kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi,” kwa muda gani? “hata ukamilifu wa dahari,”

mwisho wa ulimwengu. “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Na sasa, kwa . . . labda watazamaji, sininii . . . natumaini hakuna mmoja wao hapa usiku wa leo, lakini kama yupo, usiwe ninii, mtazamaji tu, weka imani yako pamoja na waaminio hawa. Hivi hutafanya hivyo usiku wa leo, kwa ajili ya maskini watu hawa, wagonjwa?

³⁷ Basi kumbukeni, wakati Yesu alipokuja katika nchi Yake Mwenyewe, sikilizeni yale Maandiko yasemayo, tunachukia kulisoma namna hii, bali linasema hivyo, “Asingeweza kufanya kazi nyingi kuu.” Ni vigumu kwako kuwazia juu ya Kristo kutoweza kuzifanya, bali Yeye asingeweza. Asingeweza kufanya, kwa sababu ya “kutokuamini” kwao. Alimwambia nini yule mvulana mwenye kifafa, ama, baba yake? “Ninaweza, kama ukiamini, kwa kuwa mambo yote yanawezekana kwao waaminio.”

³⁸ Ingekuwa ni furaha jinsi gani, usiku wa leo, kumwona mtu baada ya mtu kutoka kwenye viti hivi vya magurudumu, mtu baada ya mtu aliyelala hapa mahututi kwenye vitanda hivi, akiamka katika fahari ya afya na atoke nje! Si lingekuwa ni jambo zuri sana? Hao walio huko nje. . . Huyu hapa msichana mdogo ameketi, msichana mrembo, nilimwangalia jana usiku, akiketi hapa, ameketi amefungwa kwenye kiti cha magurudumu, huyu hapa mvulana mdogo ameketi hapa, huku tumbo lake limefungwa kabisa, na maskini mikono yake, na labda huenda ikawa mama yake anampepea, na jinsi moyo wa mama huyo ungeruka kwa furaha, jinsi maskini msichana huyo angejisikia, kujua kwamba kitu fulani kilikuwa kimemgusa!

³⁹ Sasa, si lazima itendeke moja kwa moja. La, la, la. Jambo pekee linalopaswa kutukia ni jambo fulani litukie moyoni mwako ambalo unaliamini. Na unapoliamini jambo hilo. . . Sasa, kuna kitu kama imani ya mbegu ya haradali, mmemsikia Yesu akinena habari zake.

⁴⁰ Sasa, mbegu ya haradali ndiyo mbegu ndogo kuliko zote, ambayo ilinenwa habari Zake. Lakini kwa nini Yeye akasema hivyo? Huwezi kuichanganyisha mbegu ya haradali, haitachanganyika na chochote. Itaninii. . . Unaweza kuchanganyia mbegu sukumawiki, na kupata chipukizi la malisho, na kadhalika, bali huwezi kuchanganya mbegu ya haradali, haichanganyiki, la, bwana, ni haradali halisi. Na kama umeninii tu. . . iwapo una imani kubwa mno, mwujiza utatendeka, lakini kama una imani ndogo tu, nayo ni mbegu halisi ya haradali, angalia ikikuleta moja kwa moja kupitia kila kisa, na kukutoa moja kwa moja nje. Unaona?

⁴¹ Kwa hiyo, sasa, usiangalie kinachokupata sasa, bali ninataka ujaribu kuwa na imani ya miujiza, ama imani ya kuponywa. Nitakuwa na imani kwa ajili yako, na kufanya yote niwezayo kukusaidia uwe na imani, kuweka imani yako. . .

⁴² Sasa, nataka tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu, na kumkaribia Mwandishi, kabla hatujalikaribia Neno Lake.

⁴³ Baba mwenye rehema, saa imewadia ambapo hatuna budi kuleta Neno hili kwenye shindano la kuamua, hatuna budi kumjaribu Mungu, kama ilivyoandikwa katika Kitabu cha Malaki, asema Bwana, “Nijaribuni,” asema Mungu. Ni changamoto jinsi gani! “Nijaribuni.” Imeandikwa kwamba inatupasa kuthibitisha mambo yote. Nasi tunasoma katika Biblia ya kwamba imeandikwa ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na kwamba aliliahidi Kanisa kwamba yale aliyofanya Yeye, Wao wangefanya baada Yake. Tunaambiwa na manabii ya kwamba kutakuwako na siku ambayo haitakuwa ni usiku wala mchana, haingeweza kuitwa wowote ule, siku yenye utusitusi, lakini wakati wa jioni inapaswa kuwa Nuru.

⁴⁴ Baba, tunajua ya kwamba ustaarabu umesafiri pamoja na jua, kutoka mashariki kuja magharibi, wale walowezi wa mwanzoni, na kadhalika. Sasa, mashariki na magharibi zimekutana, jua lile lile linalochomoza mashariki linatua magharibi. Tumekuwa na siku, Baba, ambapo tumefanya mambo makuu kwa neema Yako, tumewaongoza watu kukuamini Wewe, tangu asubuhi ile Mwana alipowaangazia watu wa mashariki, na kutoka Kwake likaja Kanisa lililojaa Upentekoste, likiwa na ishara na maajabu, huku Mwana wa Mungu akiishi ndani yao, juu ya watu wa mashariki.

⁴⁵ Sasa, juu ya . . . Hao walikuwa ni Wayahudi na Wasamaria, na Wayunani, lakini katika . . . Wamataifa ni watu wa magharibi. Nawe ulisema itakuwa Nuru wakati wa jioni. Tumekuwa na nuru ya kutosha katika siku hii yenye utusitusi kuunda madhehebu makubwa, na kuwainua wanatheolojia mashuhuri, kuwafanya watu wazaliwe mara ya pili kwa Roho wa Mungu, bali Wewe uliahidi ya kwamba Mwana yuyo huyo angewaangazia watu wa magharibi, na itakuwa katika siku hii kwamba Bwana wetu angejitambulisha Mwenyewe, Yesu aliahidi hilo, kama tu alivyokuwa wakati huo, na kungekuwako na m—mvua ya vuli, nayo ingeonekana na kuwa kama mvua ya masika, na mvua ya masika na ya vuli pia zingekuwa pamoja. Tunajua tumekuwa na majina mengi na madhehebu bandia ambayo yametokana nayo, chini yake, bali hata hivyo Neno la Mungu linadumu kweli.

⁴⁶ Sasa, Baba wa Mbinguni, tunaomba ya kwamba Maneno Yako yasiyoweza kukosea, ambayo hayawezi kushindwa . . . Naomba ujionyeshe Mwenyewe hai, usiku wa leo, miongoni mwetu, kwa kufanya na kutenda mambo uliyofanya ulipokuwa duniani, kwa sababu Wewe uliahidi jambo hilo. Nawe ulisema, ulipokuwa duniani, hukufanya lolote, isipokuwa Baba alipokuonyesha kwanza. Tunaomba ya kwamba hilo litatukia miongoni mwetu usiku wa leo, nasi tutamwona Bwana

Mungu Yehova, ambaye sisi sote tunamwabudu, jalia aje katika nguvu Zake kuu, na ataangazia utukufu Wake katika kila moyo wenye huzuni, alete imani, Uzima.

47 Tunaomba ya kwamba kila kanisa lililowakilishwa hapa liweze kuondoka hapa, usiku wa leo, likiwa na ono jipya, na roho ya uamsho ikatokee nchini humu, na mashuleni, kupate kuwa na maombi mchana na usiku, na kuona njaa na kiu. Jalia chumvi inayoyakoleza maisha yetu ije, usiku wa leo, na kutufanya sote kuona kiu ya kuwa kama Yeye. Tunaikabidhi ibada Kwake sasa, Mwandishi Yule aliyesema Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele, jalia aje akiangaza kupitia Neno Lake, na kisha alifanye Neno liangaze ndani ya watu, nasi tutamsifu kwa ajili yake kwa moyo minyenyekevu, vichwa vilivyoinamishwa. Katika Jina la Yesu, Mwanawe, tunaomba. Amina.

48 Na katika Usomwaji mtakatifu wa Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 14 na kifungu cha 27, Nimekichagua hiki kwa ajili ya mchezo mdogo wa kuigiza usiku wa leo. Nami nitaomba ya kwamba mtasikiliza kwa makini na kwa utulivu, ili kwamba kila mtu huko nyuma na kando-kando apate kusikia, kwa sababu ni vigumu, na hili jengo lina joto. Lakini ninataka kukifanya kitu kama kwenye mchezo wa kuigiza, nanii, maskini jamaa huyu hapa, ndi—ndipo wa—watoto wadogo wangeweza kufahamu dhahiri kabisa.

Mara Yesu alinena nao, akawaambia, Jipeni moyo; ni mimi; msioCOPE.

49 Ninataka kuchukua kwa ajili ya somo, *MsioCOPE, Ni Mimi.*

50 Sasa, hapana shaka ilikuwa karibu wakati jua lilipokuwa likitua, ilikuwa ni siku mbaya sana, yenye joto, umati ulikuwa umekuja kutoka kila mahali na ulikuwa umekusanyika, na wote walikuwa wamechoka na kudhoofika, nalo jua lilikuwa mbali likizama magharibi wakati ibada ilipokwisha. Nami ninaweza kuona ule mgongo mkubwa wenye misuli migumu, wa yule mvuvi mkubwa wakati akianza kusukuma mtumbwi kutoka kwenye maskini ile pwani ya Galilaya, kwenye kingo za changarawe, wakati akiusukuma majini, huku watu wamesimama ufukoni wakiwapungia mikono, wakiwasihi wote, “Rudini mkatuone tena.”

51 Basi mara ule mtumbwi uliposukumwa huko . . . Uliitwa meli siku hizo, ambayo ilikuwa ni mashua kubwa ambayo kwa kawaida ilikuwa na matanga juu yake, ndipo upepo ulipokuwa ukivuma, wangeweza kufanya safari yao haraka zaidi kwa matanga kuliko walivyoweza kwa makasia. Na katika hiyo mashua kulikuwa na . . . mvuta makasia aliketi kila upande na wakati mwingine ilichukua watu sita, au wanane, ama labda zaidi, wapiga makasia kupiga makasia, kwa sababu kweli ulikuwa ni mtumbwi wa samaki.

⁵² Nayo siku hii upepo ulikuwa shwari, kama ilivyo kawaida wakati wa kutua kwa jua, nayo hiyo Galilaya ya samawati ilikuwa nzuri na shwari. Ndipo yale mawimbi madogo yalipoanza kuelea, wakati yule mvuvi mkubwa aliposhuka katikati ya hao ndugu na kuketi karibu na Andrea, ndugu yake, akachukua makasia yake, akipangusa jasho kutoka usoni mwake, akalipungia kusanyiko mkono tena, huku maelfu wamesimama ukingoni wakipunga mikono, na kulia kwa furaha ya yale waliyokuwa wameona mchana. Mara moja moja wapiga makasia wangesimama na kupunga mikono tena, kama wale waliokuwa ufukoni, wakipunga mikono, “Rudini mkatuone tena, kwa sababu macho yetu yameona mambo makuu leo.”

⁵³ Kuna jambo fulani kulihusu, kwamba wakati. . . Watu daima wanataka kuangalia kupita pazia, mahali walipotoka, na kwamba wao ni akina nani, na wanakoenda, na kuna Kitabu kimoja tu, kati ya maandiko yote tuliyo nayo, kinachotwambia hayo, hicho ni Biblia hii. Inatwambia tulikotoka, sisi ni akina nani, na tunakoelekea. Nao walipokwisha kumwona Mwandishi wa Biblia hiyo, na walikuwa wamejua ya kwamba kwa kweli alikuwa Ndiye Yehova aliyeumba viumbe, walifurahia hilo sana, walikuwa wakiwataka warudi tena.

⁵⁴ Nao walipokuwa wakipiga makasia kupitia u—ule utusitusi, na hatimaye walienda mbali sana wasingeweza kuona mbali zaidi, basi walikuwa wakiwaaga kwa kuwapungia mikono, na labda kwaheri ya mwisho, nao wakatoweka, wakati ile meli ndogo ikisonga mbele na mawimbi madogo nyuma yake, wakati wapiga makasia wakiisukuma kwenye kilindi cha giza la Galilaya, baada ya kupiga makasia kidogo, hapana shaka ilikuwa ni kijana John, vijana wanaume kwa kawaida wana shauku nyingi kama mwanafunzi, alisimama, hapana shaka alikuwa ndiye aliyesimama, na kusema, “Ndugu, tumeingia sana baharini sasa. Nimeanza kuchoka kidogo, kwa hiyo hebu tusimame, kwa muda kidogo tu, na kupumzika.” Ndipo kila mtu akisimama, akituta hilo kasia kubwa ndani ya mtumbwi, wakaanza kupangusa jasho kutoka kwenye vipaji vya nyuso zao.

⁵⁵ Kijana Yohana akaketi kwa muda kidogo, akasema, “Ndugu,” hapana shaka alisema kitu kama hiki, “hakika tunaweza kuwa na uhakika, ya kwamba haidhuru kasisi wetu amesema nini, na yale wengi wa watu wanayowazia, hatumfuati mlokole fulani, tunamfuata Mwana wa Mungu. Kidogo nilikuwa na shaka, mpaka leo hii. Lakini nilipowaona hao watu elfu tano, wakitamani kumsikia akisema maneno machache, nao walikuwa wametoka wakaja kwenye jua hilo kali, hao akina mama pamoja na hao watoto wachanga, na jinsi walivyoketi kwa subira, wale waliokuwa na viwete, na walemavu, na vipofu, wakiwapepea, wakijaribu kusikia yale aliyosema, basi wakati wao. . . swali likatokea juu ya chakula, nasi tukamwona mvulana huyu mdogo, ambaye labda alikuwa

ameteroka shule, naye alikuwa na biskuti tano ndogo na samaki wawili wadogo, ambao . . . Akawaita, akawaketisha chini wote.”

⁵⁶ Huenda alisema kitu kama hiki: “Nilipanda juu ya mwamba nyuma Yake, kushangaa tu atakachofanya, kwa sababu nimeamini, kwa namna fulani moyoni mwangu, lakini ime—imekuwa halisi sana, hata ni vigumu kwangu kuling’amua, kuwa Mtu aliyekula pamoja nasi, na kulala pamoja nasi, na kutembea pamoja nasi, na kuzungumza nasi, naye alikuwa ni Mtu wa kawaida tu. Nami nikamwona, aliposhika hizo biskuti mkononi Mwake, hiyo mikate midogo, akaivunja, na kutukabidhi sisi ndugu, na mara mikono hiyo iliponyoshwa, kulikuwa na kipande kingine cha mkate kilichokulia kwenye huo, ambapo alikuwa amekivunja.”

⁵⁷ Ningetaka kumwuliza mwalimu wa sayansi wa shule hii, ama shule yoyote ile, kwani aliachilia atomi ya namna gani? Si ngano, bali ngano iliyokuzwa, ikasagwa, ikakatakatwa, ikaokwa, na tayari kuliwa. Alifanya nini? Na wakati alipowavunja samaki hao, samaki aliyekuwa mzazi, akazaa, akakuzwa, akatolewa magamba, akasafishwa, na kukaangwa, naye akatokea katika sekunde moja, wakati Yeye alipomfikia, alifanya nini?

⁵⁸ “Ndipo walipochukua hizo biskuti tano, na kuwalisha watu elfu tano kwa biskuti tano, na kuokota vikapu kadhaa vilivyojaa,” ninaweza kumsikia kijana Yohana akisema, “hilo liliondoa shaka lote kwangu. Kwa sababu ninakumbuka ya kwamba mama yangu Myahudi alikuwa akiniambia, loo, ninaweza kukumbuka macho yake mazuri, makubwa, ya hudhurungi yakiniangalia, na kusema, ‘Yohana, mwanangu, ninataka kuzungumza nawe juu ya Kitu kilicho halisi ambacho kitakufaidi siku moja. Katika yote utakayowahi kufanya, Yohana, shauku yangu ni wewe uwe mtu mashuhuri, lakini zaidi ya yote nataka umwamini Yehova, kama mimi na baba yako tulivyo, na tunavyojaribu kukulea.’

⁵⁹ “Nami ninakumbuka, kama mvulana mdogo, wakati macho yangu madogo yangemwangalia, naye angesema, ‘Yohana, wakati Mungu Yehova alipowahamisha watu Wake kutoka Misri, huko nje nyikani ambako hawakuwa na chakula, Yehova alinyesha mikate kutoka Mbinguni kila usiku, na kuwalisha watoto Wake wote.’

⁶⁰ “Basi, ndugu, katika mkutano huu wa ushuhuda, ningemwuliza mama yangu, ‘Mama, hivi Mungu ana Malaika wengi sana ambao ni waokaji hodari, Naye ana anga kubwa mno huko juu iliyojaa matanuri, na kila usiku Yeye angeoka mikate hiyo, na kuishusha kwa Malaika, na kuitandaza yote ardhini? Hivyo ndivyo alivyofanya, Mama?’

“Angesema, ‘La, Yohana, wewe ni mvulana mdogo tu, kwa hiyo huelewi. Yehova ni Muumba, Yeye alinena tu Neno, na

mikate ikashuka.’

⁶¹ “Sasa, ndugu zangu, alasiri ya leo nilipomwona Mtu Ambaye hula pamoja nasi mezani, Ambaye huvaa nguo kama zetu, Ambaye hulia tunapolia, hunywea chemchemi ile ile tunayonywea, ana pata potea Zake na fadhaa kama sisi, lakini nilipomwona akiichukua biskuti hiyo, akaivunja mara elfu tano, nilijua alikuwa na uhusiano na Yehova. Alikuwa Yehova yeye yule ambaye mama yangu aliniambia ambaye alileta mikate kutoka Mbinguni, kwa sababu huyu hapa akifanya jambo lile lile ambalo Yehova alifanya. Hakuwa. . .

⁶² “Kwangu mimi, tangu sasa,” kasema Yohana, “Yeye ni zaidi ya mwanadamu, Yeye ni Yehova, kwa sababu Yeye hufanya kazi za Yehova. Na sasa, hivi hatukumbuki ya kwamba Yeye alisema, ‘Nisipozitenda kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi, kama hamwezi kuamini mafundisho Yangu, basi aminini kazi nizifanyazo, na nisipozitenda kazi zile zile ambazo Yehova alizifanya, basi msiniamini Mimi?’ Na hapo akafanya kazi ile ile ambayo Yehova alifanya, na ni Yehova pekee angeweza kuifanya.”

⁶³ Kwa hiyo kwa watu, siku hizi, wanaofundisha ya kwamba Yeye hakuwa kitu ila mtu mwema, ama nabii fulani tu, Injili hiyo ya kijamii haitasimama, Yeye alikuwa ni Mungu, Muumba, akiwakilishwa katika mwili unaoitwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Yohana akasema, “Hilo lilitosha kwangu mimi.”

⁶⁴ Vema, bila shaka, mnajua Simoni, daima hana budi kuchangia sehemu yake, pia. Alikuwa ni mtu asiye na elimu, Biblia ilisema, asiye na maarifa. Hakuwa na elimu, mlango wa 4 wa Matendo unasema ya kwamba, ama, mlango wa 3 wa Matendo, naamini, ulisema kwamba yeye na Yohana wote wawili walikuwa wasio na elimu wala maarifa; nimeambiwa ya kwamba asingeweza hata kuandika jina lake mwenyewe. Lakini Yesu alimpa funguo za Ufalme, kwa sababu alikuwa na ufunuo ya kwamba Yeye alikuwa ni Nani.

⁶⁵ Alikuwa na jambo la kusema, akasema, “Vema,” ninaweza kumwona akimkumbatia Andrea, ndugu yake, na kusema, “Andrea, ninakumbuka wakati ulipokuwa ukija kuniambia kuhusu jamaa fulani aliyekonekana mshamba wa kutoka nyikani jina lake Yohana, aliyekuwa akiwabatiza watu kwa maji, akisema ya kwamba Masihi alikuwa yuaja. Vema, sasa, kama. . . Bila shaka, nisingeweza kuamini kitu kama hicho. Lakini siku moja Andrea alinishawishi nije kumsikiliza Mtu huyu, na kuona kama Yeye kweli alikuwa ndiye Masihi.” Naye akasema, “Nilikuwa nimefundishwa na baba Yangu. . .”

⁶⁶ Sasa, ningetaka tu kutoa tamshi dogo hapa. Hebu tumwigize tu kwa muda kidogo. Ninaweza kumsikia Petro akisema, “Mnajua ya kwamba nilikuwa Mfarisayo. Baba yangu alikuwa mmoja wa viongozi wa kanisa hilo la Mafarisayo, naye

baba yangu aliniambia siku moja tulipomaliza kuvua samaki, ‘Simoni, tumejipatia riziki yetu, siku baada ya siku, kutoka kwenye ziwa hili.’” Sasa sikilizeni kwa makini. “Tumejipatia riziki yetu, na, mimi na baba, na mama, na Andrea, na wote, ili kwamba tupate kuvua samaki kila asubuhi, tuliomba kwamba Mungu angetupa riziki yetu ya kila siku, atupe samaki wetu.

⁶⁷ “Siku moja wakati Baba alipoingia, na kuniketisha kwenye gubeti ya hiyo mashua, na kusema, ‘Simoni, maskini mvulana wangu, Baba daima ameamini ya kwamba siku moja Masihi angekuja katika siku zangu, sisi sote Wayahudi tumetazamia jambo hilo. Lakini labda sitamwona, ninazeeka sana. Lakini, Simoni, atakapokuja, kutakuwa na mambo mengi sana yatakayotolewa kabla hajaja ambayo yatasababisha nchi nzima kuchanganyikiwa, kutakuwa na Masihi wa uongo, na kila kitu kitakuja, lakini, Simoni, nataka ufundishwe.’”

⁶⁸ Loo, jinsi ingefaa kama sisi Wamarekani tungewafundisha watoto wetu mambo kama hayo, badala ya kucheza dansi za kurukaruka, na roki, na upuuzi tunaofanya siku hizi, na kuwaacha tu wajiunge na kanisa, bali tuwaambie cha kutarajia!

⁶⁹ Sasa, kasema, “‘Ewe Simoni, atakapokuja, nabii wetu Musa alisema ya kwamba atakuwa ni Nabii, ‘Bwana Mungu wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.’” Nasi kama Waebrania tunajulikana kuamini ya kwamba Neno la Mungu humjia nabii wala si kitu kingine. Sasa, ninawatakeni mkumbuke, Simoni, atakapokuja, Yeye atakuwa ni Nabii huyu.’

⁷⁰ “Basi nilipoenda mbele Zake mara ya kwanza . . .” Sikilizeni kwa makini, Simoni akishuhudia. Wana mkutano wa ushuhuda sasa, huko Galilaya. Basi kasema, “Nilipoenda kwanza machoni Pake, wakati Mtu huyu aliponiangalia usoni, Yeye alisema, ‘Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona.’ Si kwamba tu alijua jina langu, bali alimjua yule baba yangu mzee mtauwa. Hilo lilitosha kwangu, nilijua Yeye alikuwa ndiye Masihi, hilo lililitatua kwangu.”

⁷¹ Filipo akasema, “Je, naweza kushuhudia, ndugu zangu?” Kwa hiyo, akasema, “Nilikuwa nimesimama, na nikaona jambo hilo, sasa, Nathanaeli, usijisikie vibaya, lakini nilikimbia kumwambia Nathanaeli, kwa sababu nilijua ya kwamba Nathanaeli alikuwa ni mwanafunzi wa Biblia. Kwa hiyo nikakimbia kuzunguka mlima kumtafuta Nathanaeli, nami nikasema, ‘Nathanaeli, njoo umwone Yule tuliyemwona, Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu.’” Na huenda alisema hivi: “Nathanaeli, unajua mahali nilipokupata?”

“Naam, nilikuwa chini ya mmoja wa mitini yangu, nikiomba.”

“Naam.” Naye akasema, “Njoo, umwone Mtu tuliyemwona, nanii. . . Yesu wa Nazareti, mwana wa Yusufu, huyo ndiye yule Nabii ambaye Musa alitwambia angekuja.

⁷² “Loo, sasa!” akasema Nathanaeli. “Sasa, Filipino, ume—umeingia wazimu. Mbona, kama Masihi angekuja, ingembidi kuja kwa Kayafa kwanza, la sivyo ingemlazimu kuja kanisani mwetu. Kama Yeye—kama Yeye angekuwa Masihi halisi, unajua ingembidi kuja kwetu sisi Mafarisayo, hakuna lingine. Lakini kusema tu Yeye angetoka Nazareti, kundi la watakatifu wanaojifingirisha!” Samahani, sikupaswa kusema hivyo. Mnaona? Samahani, si—sikumaanisha hilo. Mnaona? “Asingepitia kwenye kundi la watu kama *hao*. Kama akipata kufanya jambo lolote, lingekuwa ni miongoni mwetu sisi watu werevu zaidi, kama angalifanya hivyo.” Lakini mnaona, Mungu hufanya atakalo, hiyo ni kazi Yake. Naye akasema, “Hakuna mtu angekuja namna hiyo.”

⁷³ Yeye, ndipo Filipino akampa moja ya majibu mazuri sana ambayo mtu yeyote angeweza kumpa, akasema, “Njoo, ujionee mwenyewe.” Sasa, hilo ni wazo zuri. “Usikae nyumbani na kukosoa, njoo, ujionee mwenyewe, kisha uyachunguze Maandiko, kwa kuwa Masihi bila shaka atakuwa wa Kimaandiko. Njoo, ujionee mwenyewe.”

⁷⁴ Na huku wakienda zao, ninaweza tu kuwasikia wakizungumza, basi akasema, “Je, unakumbuka vile, tulienda na kununua samaki wakati ule, naye huyo mzee mvuvi asingeweza kutia sahihi ya jina lake kwake, jamaa huyo aliyeitwa Simoni?”

“Naam, nakumbuka.”

“Wakati alipoenda Mbele za huyu Masihi, Yeye alimwambia jina lake lilikuwa ni Simoni. Basi unamkumbuka baba yake?”

“Hakika.”

“Jina lake lilikuwa nani?”

“Yona.”

“Sawa. Akasema, ‘Wewe ni mwana wa Yona.’ Sasa, Nathanaeli, wewe ni mwanafunzi wa Kimaandiko, Masihi atakuwa nini atakapokuja?”

“Atakuwa Nabii.”

“Vema, je, hilo linayatimiza?”

“Loo, naam, kama angeweza kufanya hivyo, bali siamini angelifanya.”

Ninaweza kumsikia Filipino akisema, “Isingenishangaza Yeye akikwambia wewe ni nani, utakapopanda juu.”

⁷⁵ Wakapanda juu basi, nao wakaenda mbele za Bwana Yesu, naye Yesu akaangalia pande zote akamwona, “Akasema, ‘Tazama, Mwisraeli kwelikweli ambaye hamna hila ndani yake.’” Sasa, mnasema, bila shaka, alivyokuwa amevalia. La, watu wote wa mashariki walivalia vile vile, walikuwa na ndevu, kilemba,

na kila-... ngozi nyeusi. “Kasema, ‘Tazama, Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake.’

“Yeye alisema, ‘Rabi,’” (*rabi* maana yake ni “mwalimu,”) “ulipata kuniona lini Wewe? Kabisa hatufahamiani. Ulipata kuniona lini Wewe?”

“Akasema, ‘Kabla Filipino hajakuita, ulipokuwa chini ya mtini,’” maili kumi na tano kuuzunguka huo mlima, “‘Nilikuona.’

“Akasema, ‘Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.’

“Mnakumbuka vile Mafarisayo, na waalimu walivyosema, wakisimama pale? Kasema ‘Mtu huyu ni Beelzebuli, yeye ni mpiga ramli.’

⁷⁶ “Yesu akasema, ‘Ninawasamehe hilo, lakini siku moja Roho Mtakatifu anakuja kufanya jambo lile lile, nawe ukinena neno moja dhidi Yake, halitasamehewa kamwe.’” Hiyo ni siku hizi.

⁷⁷ Sasa, ni ushuhuda wa jinsi gani! Basi hapana shaka ilikuwa ni Andrea, ninapozidi kusogea karibu zaidi na shuhuda zangu, Andrea alisema, “Naweza kushuhudia kwa dakika moja tu, ndugu? Mnakumbuka ile siku ambayo...?” Sasa, inakuwa giza zaidi na zaidi, ile nyota ya jioni ilikuwa imechomoza. Na—na kwa hiyo, kasema, “Naweza kutoa ushuhuda kidogo?”

⁷⁸ Je, huyo mama anatoka tu, hana budi...? Anatoka nje, atarudi katika dakika chache? Vema. Nilikuwa nikitaka kusema, kama yeye...msimwache aondoke bila kuombewa, tunataka kila mtu aombewe.

⁷⁹ Kwa hiyo, sasa, kasema, “Je, unakumbuka siku ile ambayo Yesu, Bwana wetu, alisema ya kwamba ilimpasa kushuka kwenda Yeriko?” Sasa, kutoka Yerusalemu hadi Yeriko, kama umewahi kuwa kule, iko moja kwa moja chini ya mlima, lakini alikuwa na haja ya kupitia Samaria. Kwa nini? Wayahudi walikuwa wamesikia, nao Wasamaria hawakuwa wamesikia.

⁸⁰ Sasa, Mataifa hawakuwa wakimtazamia Kristo yeyote. Na hebu niseme jambo fulani papa hapa, enyi wagonjwa: Yeye huja tu kwa wale wanaomtazamia. Unapozungumza habari Zake, kama vile wakienda zao kutoka Emau, na... Yeye huja tu kwa wale wanaomwamini, Yeye kamwe hatakuwa na uhusiano wowote na asiyeamini. Yeye huja tu...Na Mataifa, tuliabudu sanamu katika siku hizo.

⁸¹ Na kuna jamii tatu tu za watu, hizo ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, hapo ndipo jamii yote ya binadamu ilipotoka, na hao ni Wayahudi, Mataifa, na Wasamaria. Mwangalie Petro akiwa na zile funguo, aliufungua wakati wa Pentekoste, akawafungulia Wasamaria, akawafungulia Mataifa, ndipo ukawa wazi kwa ulimwengu. Mnaona?

⁸² Sasa, na kwa hiyo, sasa tunaona, kasema, “Alitutuma huko chini kwenye mji wa Sikari, huko, kununua chakula, vyakula. Nanyi mnakumbuka tulipokuja, tulishangaa? Mwanamke aliyekuwa na alama ya ukahaba alikuwa akienda zake kisimani, wala hapakuwapo na mtu huko. Kwa hiyo tukawazia tungeona tu yale aliyomwambia Bwana wetu, kisha tuone yale aliyofanya alipokutana na mwanamke, basi tukajificha vichakani.” Sasa, sikilizeni kwa makini hayo mao-...huo ushuhuda. “Na jambo la kwanza lililotukia wakati Yeye alipojongea pale... alijongea apate kushusha birika, chungu, achote maji, akaanza kukiinua kile chu—chungu namna *hiyo*, mbona, Yeye alisema, ‘Mwanamke, nipe maji ninywe.’

“Nasi tukawazia, ‘Vema, kwani tulimwacha Bwana wetu bila maji ya kunywa?’

“Naye akasema, ‘Mbona, tuna ubaguzi hapa, ninyi Wayahudi hampaswi kuwaomba wanawake Wasamaria vitu kama hivyo.’

“Akasema, ‘Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye, ungeniomba Mimi maji unywe, ningekupa maji usije hapa kuchota.’

“Kasema, ‘Vema, huna kitu cha kuchotea.’

⁸³ “Mnakumbuka, hayo mazungumzo yakaendelea, nasi tulikuwa tukisikiliza. Ndipo baada ya kitambo kidogo akayaangalia hayo macho yake makubwa, ya hudhurungi, na kusema, ‘Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.’ Naye huyo mwanamke akakana kabisa kwamba ana mume.

⁸⁴ “Nasi tukawazia, ‘Loo-lo! Loo, hapa kidogo amekosea. Sasa, Yeye atafanya nini? Anamwambia huyo mwanamke kwamba ana mume, ati aende akamwite mumewe, naye anasema hana mume.’ Mnakumbuka, ndugu, jinsi tulivyoangaliana?

⁸⁵ “Na ndipo tukamwona Bwana wetu katika hali Yake tulivu, huku akimwangalia mwanamke huyo usoni, na kusema, ‘Umesema kweli, kwa sababu umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako, basi ulisema vema.’ Ndipo mwanamke huyo, hivi mlikumbuka, ndugu, yale aliyosema?”

⁸⁶ Jinsi ushuhuda wake ulivyokuwa tofauti sana na wa wahubiri wa siku hizo! Hao wahubiri walisema, “Yeye ni mpiga ramli, ibilisi, Beelzebuli.” Mtu yeyote anajua kwamba kupiga ramli ni kwa ibilisi. Na hiyo ndiyo sababu Yesu alisema kunena hilo, kuita kazi ya Roho Mtakatifu upiga ramli, ama ibilisi, ilikuwa ni kumkufuru Roho Mtakatifu, na haikusamehewa, kumwita Roho wa Mungu ibilisi.

⁸⁷ Kwa hiyo basi akasema, “Mwanamke huyo alimtazama Yeye usoni, naye katika hali yake, mwenye dhambi,” (Natumaini simwudhi mtu yeyote, lakini sina budi kusema jambo fulani, na akiwa kahaba, akiishi na waume watano, waume sita, alijua

zaidi kuhusu Biblia kuliko nusu ya wasomi katika taifa hili wajuavyo.) “alisema nini? Alimkazia moja kwa moja, akasema, ‘Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii,’” sio *Beelzebuli*, kama wahubiri walivyosema, bali *nabii*. “Kasema, ‘Tunajua, sisi Wasamaria, tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atatwambia mambo haya yote, hiyo ndiyo ishara ya Masihi, atakapokuja. Tunajua, Yesu, Ambaye,’” ninamaanisha, “‘Masihi, aitwaye Kristo, Yeye atatwambia mambo haya, hiyo ndiyo ishara itakayomfuata, kwa sababu Yeye ni Nabii, Nawe huna budi kuwa nabii pia. Lakini Masihi, hatujawa na nabii kwa mamia na mamia na mamia ya miaka, kwa hiyo, lakini atakapokuja Yeye atatwambia mambo haya, huna budi kuwa Mmoja wa watumishi Wake.’”

⁸⁸ “Yesu akasema,” na Ndiye pekee ambaye angeweza kulisema, ama atakayewahi kulisema, “Akasema, ‘Mimi Ndiye,’” amina, “‘Yeye unayemwanguka, Mimi ndiye yule Masihi.’”

⁸⁹ “Akaangusha mtungi huo wa maji, alikuwa na kitu cha kuvutia zaidi wakati huo, kuliko mtungi wa maji, huyo akaingia mjini, na hivi ndivyo alivyowaambia watu wa huo mji: ‘Njoni, mwone Mtu aliyeniambia mambo ambayo nimefanya. Haimkini huyo kuwa ndiye Masihi?’”

⁹⁰ Wangesema nini leo? “Telepathia ya akili, saikolojia, msomaji wa mawazo, mpiga ramli.” Si ajabu tuna bomu la atomiki lenye jina letu. Huna budi kukataa—huna budi kuikataa rehema, ndipo hakuna kilichosalia ila hukumu baada ya kuikataa rehema, hiyo ni kweli, unavuka mpaka. Unafanya hivyo rahisi sana, watu wengi wanafikiri inawabidi kufanya jambo *kubwa*.

⁹¹ Mbona, laiti wanalijua Yohana alikuwa ni nani! Hujui kamwe mtu ni nani, mpaka wamekufa. Yeye huja kwa Kanisa teule, na hilo Ndilo pekee linalomjua. Ninawapa changamoto mrudi nyuma katika Biblia mkamtafute nabii yeyote ambaye hawamkufanyia jambo lile lile. Yesu, hawakujua Yeye alikuwa ni Nani mpaka alipokuwa amekufa, akazikwa, na kufufuka tena.

⁹² Hebu niwaulizeni ninyi Wakatoliki jambo fulani: Vipi kuhusu watakatifu we—wenu? Vipi kuhusu Joan wa Arc? Mlikuwa wasioweza kukosea kabisa. Makuhani wenu walimfanyia nini mwanamke huyo? Yeye alikuwa ni nabii mke, aliona maono, aliwaombea wagonjwa nao wakapona, nalo kanisa lenu lilifanya nini? Mlimchoma moto kwenye nguzo kama mchawi. Loo, bila shaka, mliona kosa lenu miaka mia moja na hamsini baadaye, ndipo mkafanya toba, mkachimbua miili ya hao makasisi na kuitupa mtoni, hiyo ni toba *kweli*. Inapita moja kwa moja juu ya vichwa vya wenye hekima na akili, mpaka imepita, ndipo basi tayari wako hukumuni.

⁹³ Hebu niwaambie, enyi kanisa, Roho Mtakatifu wa kweli yuko hapa katika taifa hili, usiku wa leo, katika ulimwengu huu, usiku wa leo, usimwache apite juu ya kichwa chako, mtambue sasa. Uponyaji uko hapa kwa ajili yako, Roho Mtakatifu, msamaha wa dhambi, faida zote za Kalvari ni kwa ajili yako, usizikwepe. Usijifungie kwenye fundisho fulani la kimadhehebu na kusahau kuiangalia Biblia, uone kama hii siyo ile siku tunayopaswa kuona mambo haya. Usiangalie kundi la wahubiri wasio na elimu, labda, kama mimi, ambao wanajaribu kulielezea, bali angalia yale Biblia isemayo, na uangalie kile ifanyacho. Endapo ni Roho wa Mungu, atatenda kama Roho wa Mungu, atafanya mambo aliyofanya Roho wa Mungu, asipoyafanya, basi si Roho wa Mungu.

⁹⁴ Kama nikihubiri ubatizo wa Roho Mtakatifu, ya kwamba Yesu alifufuka katika wafu, huku Mungu hathibitishi hilo kwa kazi zile zile alizofanya Yesu, basi mimi ni mwongo. Lakini kama mimi—kama nikihubiri ujumbe huo naye Mungu ageuke na kufanya jambo lile lile, kama hata sina elimu ya—ya sekondari, hiyo inaleta tofauti gani? Ni Mungu akitumia kitu fulani, Yeye anaweza kutumia kijiti akitaka, anaweza kutumia chochote atakacho, Yeye ni Mungu.

⁹⁵ Sasa, hebu na tumruhusu mwingine mmoja ashuhudie, sivyo? Hapana shaka ilikuwa ni Ndugu Mathayo, aliyesema, “Ninajua kunachelewa kidogo, ndugu, lakini hebu nitoe ushuhuda.” Kasema, “Mnakumbuka tulishuka Yeriko siku ile, mnamkumbuka maskini yule Ndugu Zakayo kule chini? Alikuwa ni mfanyabiashara, mtoza ushuru. Sikuzote tulifikiri kidogo alikuwa laghai,” samahani tamshi hilo, sikulimaanisha hivyo, “maskini haini tu. Lakini, mwajua, Dada yetu Rebekah, yeye alikuwa mwaminio Wake, alimwamini Bwana Yesu. Nanyi hivi mnakumbuka jinsi alivyowaomba wanawake wote waombe huko Yeriko, tuliposikia Yesu akishuka kwenda kufanya kampeni?”

⁹⁶ “Basi aliposhuka huko Yeriko, maskini Zakayo alitwambia baadaye, mwajua, asubuhi moja aliamka mapema, alijua Yesu alikuwa anakuja, kwa hiyo akashuka akaenda kule. Naye alikuwa maskini jamaa mfupi. Kwa hiyo, akasimama kwenye lango alipopaswa kuingilia, kwenye lango la kusini, basi akaona alikuwa mfupi sana, asingeweza kumwona. Akasema, ‘Popote nitakapomwona Jamaa huyo, nitamweleza huyo Mtakatifu anayejifingirisha ukweli wa mambo!’”

⁹⁷ Kumbukeni, Yeye aliitwa mlokole, aliitwa mwendawazimu, “Tunajua ya kwamba una wazimu, na una pepo.” Hiyo ni kweli? *Wazimu* maana yake nini? “Kichaa.” “Tunajua ya kwamba wewe ni Msamaria, una kichaa, umepagawa na pepo, huyo ndiye anayefanya mambo haya yote, wewe ni ibilisi na mwendawazimu. Hujiungi na madhehebu yetu, kwa hiyo tunajua wewe ni ibilisi.” Sasa, roho huyo angali anaishi.

⁹⁸ Sasa, tunaona ya kwamba yeye alisema, “Nitangojea tu. Rabi Lavinsky . . .” Natumaini hakuna Rabi Lavinsky hapa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

⁹⁹ “. . .? . . . Yehova anawatarajia tu kuja kanisani, na kutoa zaka zenu, na kuishi maisha mema, na hayo yanatosha. Msininii . . . Angalieni, Masihi huyo huenda akawa miaka milioni moja tangu sasa, huenda hata asije kabisa.” Kuna shule nyingi sana za Biblia siku hizi zinazofundisha ya kwamba mambo ya kimwili, ninaamini ni asilimia themanini na kitu ya *wanaojiita* Wakristo ambao hawaamini katika kurudi kimwili kwa Yesu. Nilisikia hilo; nina baadhi ya takwimu za serikali kule za madhehebu mbalimbali, nami nasahau, ni mbaya kuliko hiyo, ambao hawaamini katika kuzaliwa na bikira. Jambo lolote linawezaje kutukia? Tunawezaje kujenga uamsho katika taifa hili? Unapoondoa kuzaliwa na bikira kutoka katika Ukristo, unaubomoa msingi kutoka chini yake.

¹⁰⁰ Iwapo Yeye alikuwa ni damu ya mwanadamu, basi Yeye si zaidi ya nilivyo mimi, ama ulivyo wewe, bali Yeye ni Damu ya Mungu. Mungu, Roho Mtakatifu, alimtia uvuli bikira na kuumba Seli ya Damu, na hiyo ni Damu ya Mungu. Biblia ilisema tunaokolewa kwa Damu ya Mungu, si mwanadamu, Mungu. Lakini wanakana hayo.

¹⁰¹ “Kwa hiyo maskini Zakayo, maskini jamaa mdogo, mfupi, alisema aliamka asubuhi hiyo . . .” Hebu na tumfanyie mchezo wa kuigiza kidogo, kwa ajili ya msichana huyu mdogo aliyeketi hapa. Mwangelieni . . . Maskini macho yake maangavu, na maskini nywele zake zimechanwa chini! Nami naweza kuwazia nikiona . . .

¹⁰² “Mnajua, Rebeka, mke wake, alimwamini Yesu, kwa hiyo alikuwa tu akiomba wakati wote, ‘Ee Yesu, ninakuomba, ya kwamba wakati wowote atakapokuja mjini, hapa, kwamba maskini mume wangu mpendwa, yeye ni mtu mzuri, lakini yeye amejifunganisha tu nao, kila namna ya mikutano ya Kiwanis, na karamu za vyama, na mambo haya yote kwa . . .”

¹⁰³ Sasa, sisemi chochote juu ya Kiwanis sasa, hicho ni sawa. Mnaona? Baadhi tu ya watu huchukua . . . Kweli ni—ninaamini ya kwamba Wamasoni wako sawa, lakini Chama cha Masoni kamwe hakitapachukua mahali pa Kanisa, ama Damu ya Yesu Kristo. Jamaa zangu wote ni Wamasoni, na, sasa, wako sawa kama chama, bali haitachukua mahali pa Kanisa. Nayo shida yake ni kwamba, mmelifanya kanisa, si zaidi ya chama cha Masoni, ama chama kingine chochote, kanisa ni nyumba ya Mungu ambamo Kristo anaishi, na kujidhihirisha Mwenyewe miongoni mwa watu. Hiyo ni kweli.

¹⁰⁴ Angalieni, “Kwa hiyo Zakayo, yeye, ninamwona akienda huko nje, naye akasema, ‘Sasa, hapa wanapanda kila mahali malangoni na kadhalika, Ni—nisingeweza kumwona kamwe,

kwa hiyo ninashuka kwenda hapa chini, ninajua Yeye sikuzote hushuka kwenye Barabara ya Haleluya,” Angali anafanya hivyo, “kisha huingia kwenye Barabara Kuu ya Utukufuni, na kwa hiyo ninashuka kule chini pembeni nikamngojee.’

¹⁰⁵ “Kwa hiyo anashuka kwenda kule, naye amevaa vazi lake lililo bora sana, mwajua, alikuwa amesimama kule chini pembeni na vazi lake lililo bora sana, amejinadhifisha sana, mwajua, ‘Ngojeni mpaka nitakapomwona yule pale *anayejiita* Nabii kutoka Galilaya! Nitamwambia ukweli wa mambo nitakapomwona. Hajui nina digrii ngapi, naye rafiki yangu mwema, rabi, amenifundisha mambo mengi, nitamwambia jambo fulani. Nami nitamwambia kama hataachana na uchawi Wake kwa mke wangu, nitamtendea Yeye kitu. Nitamwambia ukweli wa mambo. Huku mke wangu yuko huko nje kwenye mikutano mirefu ya maombi ya usiku kucha, na kadhalika, la, bwana. Aliiacha klabu, akaacha kucheza karata, ameachana nayo, loo, jamani, wana nanii wote. . . mke wa rabi, na hao wote, wote, ama, watu hawa wengine, wote wamechanganyikiwa, nawaambia, kwa huo ulokole. Nitamwambia nitakapomwona!’

¹⁰⁶ “Akiwa amesimama pale akiunadhifisha maskini mwili wake, aliwazia, ‘Ngoja kidogo, umati ule utamfuata.” Hiyo ni kweli, kwa kawaida wao hufanya hivyo. “Umati ule utamfuata, kwa hiyo kama akija *hapa* juu, vema, sitakuwa bora kuliko nilivyokuwa *kule* chini.’ Kwa hiyo anasema, ‘Mnajua kile ninachoamini nitafanya, kuna mkuyu umesimama pale, kwa hiyo ninaamini nitapanda tu kule juu. Nitakapofika juu kwenye mti huo, nitamwambia atakapopita.’

¹⁰⁷ “Kwa hiyo anaangalia pande zote, na kusema, hilo hapo pipa la takataka ya mji, ‘Vema, labda, kama ningeweza kulileta hilo hapa! Siwezi kuuparamia huu mti.” *Paramia*, nilimaanisha “panda juu ya mti.” Mnaona? Samahani lugh- . . . ama, ninii yangu. . . mimi ni Mkentaki tu. “Kwa hiyo— kwa hiyo anaenda pale na kuushika. . . Sasa, sasa, anarudi nyuma, ‘Mwajua, jamani, nimevaa nguo zangu zilizo nadhifu sana. Ninawezaje. . . ? Nisingeweza kushikwa na pipa hilo la takataka.”

¹⁰⁸ Lakini kuna *jambo fulani* kulihusu, kama unajaribu kumwona Yesu, utaweza kwa njia fulani kumwona. Iwapo wewe. . . Utafanya mambo ambayo hukudhani uliyafanya, hukuwazia kamwe ungefanya hivyo, bali utayafanya kwa vyovyote vile, kama unataka kumwona Yesu. Hebu kaa mahali baadhi ya watu hawa walipo, nawe utapoteza tu maskini sifa hizo zote.

¹⁰⁹ “Kwa hiyo ananyemelea pale, na kushika pua yake, na kuchukua hiyo ndoo ya takataka.” Unaelewa, kipenzi? “Huyu hapa anakuja, mwajua, ameibeba, ndipo ikawa aliangalia juu, na huyu hapa mshindani wake, akisema, ‘Naam! Mnajua nini?’

Yule pale Zakayo, yeye ni mfanyakazi wa jiji sasa, kazi ya kuzoa takataka.' Vema, aliazimia kumwona Yesu, kwa hiyo hakujali."

¹¹⁰ Labda baadhi yenu nyote mnaweza kujisikia vile vile, daktari fulani wa uungu aketi kule nyuma aseme, "Nisingetaka kushikwa miongoni mwa kundi hili la watu," lakini umeanikwa sasa, ndugu, umeangamizwa sasa. Lakini kama umedhamiria kumwona Yesu, hujali kwa vyovyote vile, hiyo ni kweli, hujali kwa vyovyote vile.

¹¹¹ "Huyu hapa anakuja na ndoo ya takataka, anaenda pale, na kuiweka chini karibu na mti, kisha anauparamia huo mti, naye anapanda pale juu, anaketi pale akichokoa vibanzi mkononi mwake, akipangusa takataka kwenye nguo zake mpya. Lakini anataka kumwona Yesu.

¹¹² "Akasema, 'Unajua nini? Ninakumbuka Rebekah aliniambia ya kwamba Jamaa huyo alikuwa ni Nabii. Sasa, ninaamini kuna udanganyifu katika hilo, mahali fulani.'" Wangali wanaamini jambo lile lile. "Kuna udanganyifu ndani yake, mahali fulani. Hao wanafunzi, kwa namna fulani, wanabuni miongoni mwao, *jambo fulani*, wanaenda na kumchukua mtu ambaye Yeye anamjua, Naye anawaambia mambo hayo. Kwa hiyo ni—ninajua. . . Mnajua nini? Nitawaambia nitakalofanya, nitajificha tu kutoka kwa Jamaa huyo.'

¹¹³ "Kwa hiyo akaketi mahali ambapo matawi mawili yanakutana." Nawe unajua, hapo ni mahali pazuri kwako kuketi kwa muda, ambapo njia mbili zinakutana, yako na ya Mungu, ujiamulie kutoka hapo. "Kwa hiyo, akaketi kwenye tawi hili, kisha akanyosha mkono na kushika baadhi ya huo mkuyu mkubwa," *mkuyu*, kwa kweli ulikuwa ni mzeituni, "kwa hiyo akayavuta tu, na kujifunika kila mahali, kasema, 'Kamwe hataniona nimeketi hapa juu, bali nitamwangalia atakapopitia hapa.' Anajifunika kila mahali, kisha anaacha jani moja kubwa pale, apate kuliinua na kuchungulia nje," namna *hii*.

¹¹⁴ "Kwa hiyo anaketi pale, naye akasema, 'Sasa, nitaweza kujua, kwa sababu *kwa namna fulani*, kila mahali alipo kuna kelele nyingi sana.'" Mwajua, hilo halijabadilika. La. Alipo Yesu, kwa kawaida kuna kelele nyingi sana. "Kwa hiyo, akasema, 'Nitasikia kelele zikija muda mrefu kabla hajafika pale.'

¹¹⁵ "Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo akasikia kelele. Nanyi mwajua, huyu hapa anatangulia, jamaa mkubwa mno, mwenye nguvu, Simoni Petro, akisema, 'Mwaweza kusimama kando? Tunasikitika sana. Bwana wetu amechoka, alihubiri karibu usiku kucha, jana usiku; aliwaponya wengi wa wagonjwa. Mwaweza kusimama kando, tafadhalini? Tunasikitika. Watu pamoja na watoto wao, vema, mwaweza kusimama tu kando, tafadhalini? Bwana wetu hana budi kula kiamshakinywa Chake, bado, asubuhi ya leo. Mwaweza kusimama tu kando?'

116 “Kwa hiyo Zakayo akasema, ‘Huyo si Yeye, huyo ni yule mzee mvuvi asiye na elimu kule juu niliyekuwa nikinunua samaki kwake, huyo si Yeye.’ Kwa hiyo yapata wakati huo, akasema, ‘Hana budi kuwa ni Jamaa mkubwa mno, wa kifalme, amevikwa taji kichwani Mwake, akitembea imara, mwajua.’” Mwajua, ninachukia kuona mtu akikigamba, hicho ni kiburi, huyo—huyo si mtu wa Mungu. Kwa hiyo hapa, lakini waliona wakati alipokuja, Jamaa mdogo, mnyenyekevu, sio na ukosi uliopinduliwa hapa nyuma, na vilemba kichwani Mwake, bali alikuwa ni Mtu wa kawaida tu, amevalia kama mtu wa kawaida.

117 “Kwa hiyo wakati akipitia hapo, Zakayo akavuta jani lake chini, kasema, ‘Unajua, kuna *kitu fulani* tu kuhusu Mtu huyo ninachokipenda.’” Kamwe huwezi kumtupia jicho pasipo kumpenda, sijali ni nani. Ninajua mara ya kwanza nilipoangalia, kwa imani nilimwona, kile alichokuwa, nikaweka mikono yangu miguuni Mwake, nikamwona akifa pale kwa ajili yangu, na kunitazama, loo, hilo lilitosha.

118 “Zakayo akavuta jani lake chini, kasema, ‘Loo, amekaribia? Sasa, Yeye hawezi kuniona, hatajua niko hapa. Sasa, Yeye hajui, kwa sababu Yeye, kama angeniona hapa juu...ila hawezi kuniona, maana nimefunikwa kabisa, niko kwenye mti huu, na maskini jamaa mdogo nikiketi kwenye tawi hili hapa, nami nitamtazama.’ Kwa hiyo, tulimwona, Yeye alikuja akitembea, katika njia Yake tu ya kawaida, akitembea kwa utulivu, anashuka chini.” Ninaweza kumwona maskini Zakayo akiangalia chini ya jani la mti, namna *hii*, mwajua, akimtazama Yeye alipokuwa akipita.

119 “Mara alipopita tu, akainua jani lake, Yesu akasimama, akasema, ‘Zakayo, shuka chini. Naenda nyumbani pamoja nawe kwa chakula cha kutwa.’ Si kwamba tu alijua alikuwa pale juu, bali alijua jina lake lilikuwa nani, hilo lilitosha.

120 “Vema,” kisha akasema, “mnakumbuka tulipokuwa tukitoka langoni, Bartimayo Kipofu, wakati Bartimayo Kipofu aliposema alikuwa ameketi pale, akiwazia jinsi ambavyo kwamba—ambavyo Masihi angekuwa wakati atakapokuja, na kadhalika, na jinsi ambavyo kama manabii waliishi, angewaendea na kuwaomba, apate kuona, ndipo mara akawasikia wakipita, umati wenye kelele? Sisi hao hapo tena. Naye alikuwa ameketi hapo, akitetemeka kwa baridi. Mnaukumbuka ushuhuda wake? Basi akasema—akasema, ‘Ni nani anayepita?’

“Kisha kasema, kila mtu akasema, ‘Loo, nyamaza.’

121 “Ndipo akamsikia mtu fulani akipaza sauti, ‘Aisee! Aisee, wewe! Wewe, nabii wa Galilaya, wewe! Tunasikia ati unawafufua wafu,’ ilikuwa ni kuhani, kasema, ‘tuna makaburi yote yaliyojaa hao hapa juu, njoo ukatufufulie mmoja, tutakuamini.’” Maskini ibilisi yuyo huyo angali hai, mwajua. “Tulisikia unawafufua wafu, tuna makaburi yaliyojaa

wenye haki waliokufa hapa juu, hima, ukamfufue mmoja wao, tutakuamini.”

¹²² Halikumsumbua hata kidogo, Yeye aliendelea tu kutembea. Nafsi za ulimwengu zilikuwa juu Yake, alikuwa akienda Kalvari wakati huo, akipanda kilima.

“Bartimayo akasema, ‘Ni nani anayepita?’ Nao wakamsukuma akaanguka.

“Ndipo baada ya kitambo kidogo mama fulani mzuri, mwenye adabu akaja, na kusema, ‘Loo, maskini jamaa!’ Kasema, ‘Loo...’

“Kasema, ‘Ni nani anayepita, mama?’

“‘Loo,’ akasema, ‘hivi hujui ni Nani?’ Kasema, ‘Ni Yesu wa Nazareti.’

“‘La, sijui Yesu wa Nazareti ni Nani...’

“‘Yule Nabii wa Galilaya?’

“‘La, sijawahi kusikia kuna Mtu kama huyo.’

“‘Unajua Mwana wa Daudi atakuwa Nani?’

“‘Loo, Masihi?’

“‘Naam.’

“‘Loo, laiti ningalimwona tu Yeye! Unajua ndivyo ilivyo?’

“‘Mimi ni mmoja wa wafuasi Wake.’

¹²³ Nami nataka kusema jambo fulani hapa: Wafuasi wake daima huonyesha adabu kwa kila mtu maishani mwao, mnaona. Wako tayari kumsaidia mtu, tayari kufanya jambo kwa ajili ya mtu mwingine, wafuasi Wake wa kweli.

“Naye akasema, ‘Naam.’” Na huenda ikawa, hebu tuseme ilikuwa ni Rebekah, “‘Mume wangu ndio kwanza aokoke muda mfupi uliopita, nami nimejaa furaha sana.’

“‘Vema, sasa, unamaanisha ya kwamba Huyo ndiye Masihi ambaye tumefundishwa kwamba atakuja, yule Nabii ambaye Musa alisema? Yuko umbali gani?’”

¹²⁴ Sasa, kama uliwahi kuwa huko, na kuangalia mahali alipodhaniwa ameketi, alikuwa kwenye umbali wa yadi mia mbili na hamsini, huku yapata watu elfu nne ama tano wakipiga mayowe, “Hosana, kwa Nabii! Hosana, kwa Nabii!” Mwingine akipaza sauti, “Mwondoeni!” Na kumtupia matunda yaliyooza, na vitu kama hivyo. Mambo hayo yote ya namna hiyo, angewezaje kusikia, “Yesu, Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu! Ewe Mwana wa Daudi, unirehemu?”

¹²⁵ “Kwa hiyo hebu na tuwazie ya kwamba Bartimayo aliwaza hivi: ‘Kama Yeye ndiye yule Masihi, Yeye ni Nabii.’ Ninaweza tu kumwona akipiga magoti, akitetemeka, na kusema, ‘Loo, Yehova, Masihi Wako ambaye ninatamani kumwona maishani mwangu mwote, na kama huyo Ndiye anayepita, jalia nimguse,

Bwana. Siwezi kumfikia, lakini hivi imani yangu yaweza kumfikia? Loo, jalia nimguse, Bwana!’

¹²⁶ “Yapata wakati huo Yesu akasimama, na kusema, ‘Mleteni hapa.’ Asingeweza kumsikia, Yeye alikuwa mbali sana naye, umati huo wote unaopiga kelele, lakini imani yake ikamsimamisha.” Basi angalieni mahali alikokuwa akienda, Yerusalemu akiwa na dhambi za ulimwengu juu Yake, lakini tazameni, imani ya ombaomba mmoja kipofu, amina, ilimsimamisha. Nayo imani ya mtu mmoja hapa, usiku wa leo, itamleta kutoka Utukufuni, huku chini, kufanya jambo lile lile.

¹²⁷ Loo, tungeweza kuendelea na huo ushuhuda, bali sina budi kuharakisha. Naam, nimepitisha wakati. Hebu tu nimalizie maskini tamshi moja zaidi. Walikuwa wakashuhudia. Mnajua nini? Wakati hao ndugu walipokuwa wakashuhudia, ilitokea kwamba ibilisi aliangalia juu ya uzio wa ngazi, huko mahali fulani, ama upande wa pili wa kilima, na kusema, “Loo-lo! Loo-lo! Nimewapata sasa, waliondoka bila *yeye*.” Na hivyo ndivyo kanisa limefanya siku hizi. Tumekuwa na miradi mikubwa sana ya ujenzi, pesa nyingi sana, mitindo mingi sana, tukijaribu kujifananisha na watu wengine, mpaka ninahofia tumeondoka bila Yeye, maisha yetu yanathibitisha hilo, tumeondoka bila Yeye.

¹²⁸ Ibilisi anasema, “Sasa, ninaweza kuwapata.” Kwa hiyo akaanza kupuliza pumzi yake ya sumu, bahari ikaanza kushuka moja kwa moja mpaka chini, huku mawimbi makubwa yakipiga. Hivyo ndivyo afanyavyo siku hizi wakati anapokuona ukiondoka bila... kanisa lenye lundo tu la theolojia baridi, ya kawaida; “*Amina*” moja, ingemfanya mtu fulani, kuinua kichwa chao pande zote, wakashangaa imekuwaje; hakuna roho, hakuna tena mikutano ya maombi ya usiku kucha, hakuna mzigo tena kwa ajili ya wagonjwa, hakuna mzigo tena kwa wanaokufa, hakuna mzigo tena kwa ajili ya wenye dhambi; ndipo akaanza kupuliza pumzi yake ya sumu, akisema, “Pia siku za miujiza zimepita.”

¹²⁹ Akaanza kuiyumbisha hiyo mashua ndogo huku na huku. “Je, ni halisi? Je, ingeweza kuwa halisi? Labda tumekuwa makosani. Labda baba zetu, waliosema tumpokee Roho Mtakatifu, labda ni kosa. Wesley kidogo angeweza kuwa amerukwa na akili, Luther angeweza kuwa amekosea pia, Knox, Calvin, jamaa hao wote.”

¹³⁰ Naye John Wesley alihubiri uponyaji wa Kiungu, na kuamini katika uponyaji wa Kiungu, na kuweka uponyaji wa Kiungu katika matendo. Kila wakati tulipopata kuwa na uamsho, wakati wowote kote katika historia, ulianza na uponyaji wa Kiungu. Hiyo ni kweli. Angalieni kama Luther hakuponya, hao wengine, kote kote chini, walifanya uponyaji wa Kiungu. Ndipo wakauunda dhehebu, na ndipo upepo ukaanza kuvuma, maana

unapouundia dhehebu unaondoka bila Yeye, ndipo una theolojia yako mwenyewe basi, unaona.

¹³¹ Kama ungefanya fundisho lako, na kulimalizia kwa koma, “Tunaamini *hili*, *pamoja* na kadiri Mungu atakavyonifunulia,” hilo ni sawa. Lakini unapoandika fundisho lako, unalimalizia kwa nukta, “Tunaamini *hili* na *hilo* pekee,” basi umemfungia Mungu mumo humo nje ya nukta hiyo. Kweli. Mungu anaendelea tu kusonga mbele, Yeye anasonga mbele tu.

¹³² Ile Nguzo ya Moto, mara Luther alipoiona, alitoka kwenye kanisa Katoliki. Walifanya nini baada ya kifo cha Luther? Waliunda madhehebu chini Yake, ule Moto ukaondoka. John Wesley akauona, akamiliki utakaso, akatoka akaufuata, akamwacha Luther, akawaacha Waanglikana, kisha akaufuata. Walifanya nini baada ya Wesley, na Asbury, na hao wengine walipokufa? Waliunda dhehebu, Mungu akaondoka moja kwa moja, akawaendea Wapentekoste. Hapa wakaliona, nao wakaondoka pamoja na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ninyi nyote mlifanya nini? Kuliundia dhehebu, Naye anajiondoa moja kwa moja kwenu, anaendelea mbele moja kwa moja. Mnaona?

¹³³ Anaendelea tu moja kwa moja, maana mnaanza kupigana na kugombana ninyi kwa ninyi. Mnapofanya hivyo, mmekwisha, mmekwisha, ndugu. Mungu ni upendo, “Hivi watu wote watajua ya kuwa ninyi ni wanafunzi Wangu, mkipendana ninyi kwa ninyi,” huku mmenyosha mkono na kutoa moyo. Baadhi ya watu walio bora sana ulimwenguni wako katika makanisa haya, lakini mfumo wa kitu hicho, mnaona, ndio unawapata. Watu wazuri katika kanisa Katoliki, bali mfumo ndio unaowazuia kumtumikia Mungu.

¹³⁴ Sasa, Yeye aliwaona, nao hao hapo, wakirushwa-rushwa, matumaini yote yamekwisha. Hapo ndipo ulipo, mahali ulipo, maskini mwanadamu huyu aliyelala hapa, mahututi, mtoto huyo mchanga, ninyi huko nje mlio na ugonjwa wa moyo, mlio na kansa, hapo ndipo mlipo, matumaini yote karibu yamekwisha. Lakini mnajua nini? Katika dhambi zetu zote, katika tofauti zetu zote, hebu nitoe neno hili la kuhuisha kabla hatujaomba: Yeye hakuwa amewaacha, alipanda mlima mrefu kuliko yote iliyokuwepo, kusudi aweze kuwaangalia kote kote, alikuwa ameketi pale akiangalia.

¹³⁵ Wakati alipokufa pale Kalvari, ndugu, Yeye hakutuacha kamwe, alipanda kilima cha Kalvari, akaendelea na kupita mwezi na nyota, mbele na juu ya Njia ya Kilimia Cheupe, mpaka akaketi mkono wa kuume wa Mungu Mbinguni. “Nalo jicho Lake liko kwenye shorewanda,” nami ninajua Yeye anatuangalia, usiku wa leo. Hakuwa ameenda mbali sana, akawaona katika shida, aliona ibilisi alikuwa karibu kuwashika.

¹³⁶ Anaona ibilisi yuko tayari kuwashika ninyi nyote, Yeye anaona karibu yuko tu tayari, mnaenda kwenye kaburi

la mapema, baadhi yenu mnaenda kama mwenye dhambi, msipotubu, baadhi ya hawa wataondoka kabla ya wakati wao, kwa sababu ugonjwa wa Shetani umeingia, ukiunyakua uhai kutoka kwenu. Lakini kumbukeni, Yeye ameketi huko Juu akiangalia, akingojea kulithibitisha Neno Lake, Yeye hulilinda apate kulithibitisha. Hiyo ni kweli?

¹³⁷ Ilikuwa? Wakati makasia yalipokuwa yamevunjika, nguzo ya mlingoti ikawa imeanguka, maskini meli hiyo ilijaa maji... Hiyo ni karibu kama vile makanisa yetu yalivyojaa maji usiku wa leo, tukibishana kuhusu mabatizo ya kila namna, na kadhalika, tumejaa maji. Kubatiza namna *hii*, kunyunyizia, kumwagilia, kugombana, kubishana, kufanya yasiyofaa, makasia yamevunjika, na matanga yamepasuka, wala hakuna tena upepo unaoenda kasi, kama ungekuja usingeweza kutupulizia popote. Haya basi, unaona, yote yamekwisha.

¹³⁸ Lakini huyu hapa anakuja akitembea juu ya maji, loo, jamani, akitembea juu ya maji. Nao wanafunzi waliwazia nini walipomwona akija akitembea? Walidhani Yeye alikuwa ni mzuka, wakasema, “Loo, ni mzimu. Loo, tunaogopa! Tunahofu!” Ndipo wakaanza kulia, “Loo, ni mzuka! Usijihusishe nao. Ni—ni—ni—ni telepathia ya kiakili. Ni—ni—ni upiga ramli.”

¹³⁹ Kama tu walivyofanya wakati huo, ndivyo wanavyofanya siku hizi, jambo lile lile, wanaogopa, “Vema, kanisa letu halifundishi hilo, ninaliogopa.” Lakini Biblia inafundisha hivyo. Kama angeweza kuzungumza usiku wa leo, mnajua angesema nini? “MsioCOPE, ni Mimi.” Na kama ni Yeye, Yeye atafanya kazi Zake zile zile, Yesu alisema, “Nisipozitenda kazi za Baba Yangu basi msiniamini Mimi, bali nikizitenda kazi za Baba Yangu, basi ziaminini hizo kazi.”

¹⁴⁰ Kama niliwaambia, sikilizeni, katika kufunga, kama niliwaambia roho ya msanii ilikuwa ndani yangu, vema, mngenitarajia nitoke hapa nje na kuchora picha kama huyo msanii, endapo roho huyo yuko ndani yangu. Hiyo ni kweli? Kama niliwaambia roho ya makanika ilikuwa ndani yangu, mngetarajia nifahamu mdundo wa motokaa hiyo, karibu hivyo, shida yake. Kama niliwaambia roho ya John Dillinger ilikuwa ndani yangu, ningekuwa na bunduki, ingekuwa ni hatari kusimama mbele yangu, iwapo roho huyo alikuwa ndani yangu. Kama niliwaambia Roho wa Yesu Kristo alikuwa ndani yangu, basi nitafanya kazi za Yesu Kristo, vivyo hivyo na Kanisa Lake, maana huo ni Uzima Wake ndani Yake.

¹⁴¹ Sasa, kile alichokuwa wakati huo, na kile hao watu walichoshuhudia, endapo Yeye atafanya jambo lilo hilo, usiku wa leo, hivi utatambua ya kwamba imani yako imemwita kutoka Utukufuni hadi kwenye jengo hili, usiku wa leo? Utalikubali?

Basi mngesemaje? “Msiogope,” hivyo ndivyo Yeye angesema, “Ni Mimi.”

¹⁴² Baadhi yenu mnasema, “Ni kitu gani, Ndugu Branham?” Mimi—mimi. . . Kila usiku wakati mkutano unapoanza, ninawahisi wakisema, “Mwajua, ninaamini anasoma mawazo yao,” mmoja anasema, “Ni telepathia,” mmoja anasema, “Ni upuuzi,” ndugu, unatia tu muhuri maangamizi yako mwenyewe.

¹⁴³ Kama angeweza kunena Mwenyewe. . . Kama hilo si Neno lile lile Yeye. . . Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yesu Kristo ni Neno la Mungu? “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Hiyo ni kweli? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Waebrania, mlango wa 4, Biblia ilisema ya kwamba Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili? Hiyo ni kuhubiri, kumkata kabisa, kukata zote mbili, pande zote mbili, likija na likienda.

¹⁴⁴ Baadhi ya watu hufikiri unyenyekevu ni kitu kinachopaswa kuvalia sketi. La, la, m—mnaelewa hilo vibaya. Yesu, Mtu mnyenyekevu kuliko wote aliyepata kuishi, Naye angeweza kusokota kamba, na kuwaangalia kwa hasira, na kuwafukuza kutoka hekaluni. Naam, bwana. Bila shaka.

¹⁴⁵ Unasema, “Alikuwa na huruma.” Naam. Kwa nini akapitia katika maelfu ya watu waliokuwa viwete, vipofu, vilema, waliopooza, na kumwona mtu aliyelala kwenye godoro? Labda alikuwa na ugonjwa wa tezi dume, angeweza kutembea, alisema, “Ninaposhuka, mtu fulani ananipita.” Yeye. . . Haukuwa unaenda kumwua, alikuwa nao miaka thelathini na minane. Nayo Biblia ilisema Yeye alipitia katika umati mkubwa wa viwete, vipofu, vilema, na waliopooza. Hiyo ni kweli, ndugu? Mungu mwenye huruma, akipitia kati ya watu wa namna hiyo, na kumwona mtu amelala kwenye godoro.

¹⁴⁶ Ni wangapi wanaojua godoro ni nini? Nililelewa kwenye moja, mnaona, kwa hiyo. . . Halafu, wewe. . . Amelala kwenye godoro hili, naye huyo hapo, amelala pale, ndipo Yesu akaangalia kote mpaka akamwona, nayo Biblia ilisema ya kwamba Yeye alijua alikuwa katika hali hii, ndipo Yeye akasema, “Wataka kuwa mzima?” Mbona si yule aliyepindika? Vipi kuhusu mwanamke huyo hapo pamoja na mtoto mchanga mahututi? Vipi kuhusu hawa? Vipi—vipi kuwahusu? “Wataka kuwa mzima?”

Akasema, “Sina mtu wa kuniweka majini, ninapokuja, mtu fulani ananitangulia.”

Yesu akasema, “Umekuwa nao kwa muda wa miaka thelathini na minane.”

“Hiyo ni kweli.”

“Vema. Jitwike godoro lako, uende nyumbani mwako.” Kamwe hakuuliza swali, alichukua tu hicho kitanda akaondoka. Hiyo ni kweli?

Nao Mafarisayo na Baraza la Wazee, kanisa, wakamwuliza swali, “Mbona sio hawa wengine wote?”

¹⁴⁷ Akasema, “Amin, amin, nawaambia, naweza... Mwana hatendi neno Mwenyewe, bali lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile.” Hiyo ndiyo huruma. *Huruma* ni “kufuata mapenzi ya Mungu,” sio kusikitika kwa binadamu, bali *huruma*. Loo, ni maneno mawili tofauti kabisa, *kusikitika*, na *huruma*. Mnaona? Kama sivyo, Yesu hakika alifanya kosa fidhuli alipofanya hivyo. Mnaona?

¹⁴⁸ Kwa hiyo, inawabidi kutambua ya kwamba Kristo mwenye huruma, tena, amemponya kila mmoja wenu, nyote mko huru, kama mnaweza kuamini. Sasa, mnaamini hili ni Neno la Mungu? Kwamba hivyo ndivyo hasa Yesu alivyofanya, kile walichokuwa wakishuhudia? Inueni mikono yenu.

¹⁴⁹ Sasa, kama Yeye angekuwa amesimama hapa, Yule aliyeliandika Neno, kama angekuwa amesimama hapa, na angewaambia, na kuwathibitishia ya kwamba alikuwa amesimama papa hapa jukwaani, ungekuwa tayari kumkubali, na kusema, “Hilo latosha kwangu, mimi...”? Kama Yeye amesimama hapa, na aliandika Neno, na kusema, “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao, na kazi nizifanyazo Mimi, hao nao watazifanya...” Hiyo ni kweli? Yohana Mtakatifu 14:7...14:8 “Kazi nizifanyazo...”

¹⁵⁰ Sasa, hii hapa changamoto kubwa mbele ya, kama vile ndugu alivyosema, watu elfu moja mia tisa, hii *hapa* Biblia kwenye dawati, *hizi* hapa karatasi mbili ama tatu za namna fulani, na kitu fulani, hata sijui ni kitu gani kilicho juu yazo, ni za baadhi ya ndugu hapa, hii *hapa* Biblia, kuna watu elfu moja mia tisa, hakuna mtu hapa ninayemjua. Siwezi kuona mwanadamu mmoja aliye hai ninayemjua katika kusanyiko hilo. Endapo nyinyi nyote ni wageni kwangu, inua mkono wako.

¹⁵¹ Ningetaka hata, labda, kama ningekuwa na wakati, kumchukua mhudumu huyu, aliyekuwa kwenye moja ya mahojiano ya faragha asubuhi ya leo, nimwache asimame na kuwaambia yale Roho Mtakatifu aliyofanya huko juu asubuhi ya leo, bila shaka yoyote yale aliyofanya, na karudi, na kutoa, na kuonyesha, na kufunua, na... Lakini kama mnaamini ya kwamba Yesu Kristo anaishi ndani ya watu Wake...

¹⁵² Angalieni, yote aliyokuwa Mungu, aliyamimina ndani ya Kristo. Mnaamini hilo? “Katika Yeye ulikaa utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili.” Mnaamini hilo? Maana Yeye alikuwa—Yeye alikuwa—Yeye alikuwa Mungu katika... Alikuwa ni Mwana wa Mungu, bali hata hivyo alikuwa Mungu, Mungu alibadilisha

kinyago chake kutoka kwa Roho, na kuitandaza hema Yake, na kuanza... Yeye akafanyika sisi. Alifanyika sisi, kusudi sisi, kwa neema Yake, tupate kuwa Yeye. Amina. Ndugu, hakika, wanapata hilo. Mnaona?

¹⁵³ Mungu alifanyika mwili, ili tuweze... Timotheo wa Kwanza 3:16: “Bila shaka siri ya utauwa ni kuu, kwa maana Mungu alidhihirishwa katika mwili, na kuaminiwa ulimwenguni, na—na ameondoka na amepokelewa juu Utukufuni.” Mungu aliyedhihirishwa.

¹⁵⁴ Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake. Kwa hiyo yote aliyokuwa Mungu, aliyamimina ndani ya Yesu, na yote aliyokuwa Yesu, aliyamimina ndani ya Kanisa. Kwa hiyo hiyo ndiyo sababu Yeye alituagiza tubatize, kasema, “Enendeni basi, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Kwa nini? Si Miungu watatu mbalimbali, bali ofisi tatu za Mungu yeye yule, Ubaba, Uwana, kipindi cha Roho Mtakatifu. Sasa, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, huyo ni Mungu. Si Miungu watatu ama wanne ama watano mbalimbali, bali Mungu mmoja aliyedhihirishwa katika madhihirisho matatu ya Mungu mmoja, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, utatu.

¹⁵⁵ Sasa, tunaona Mungu yuyo huyo basi, aliyekuwa katika Nguzo ya Moto, alikuwa ni yeye yule aliyekuwa ndani ya Yesu, kwa sababu Yeye alisema, “Ibrahimu asijakuwako MIMI NIKO. Mimi ndiye ule Mwamba uliokuwa nyikani.” Naye akasema, “Nimetoka kwa Mungu, na ninaenda kwa Mungu. Siku hiyo, mtajua ya kwamba Mimi ni Baba, Baba ndani Yangu, Nami ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Haya basi, sote pamoja, Mungu ndani yetu, Mungu ndani yako, Mungu yule yule.

¹⁵⁶ Shida yake ni kwamba, ninyi Wapentekoste, ninyi Wabaptisti, ninyi Wamethodisti, mnashindwa kutambua majaliwa yenu mliyopewa na Mungu. Nisikieni! BWANA ASEMA HIVI, amini kwa moyo wako wote. Aliahidi jambo hilo katika siku za mwisho. Halijakuwako kwa miaka elfu mbili, kwa sababu Biblia ilisema halingekuwako. Lakini Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma,” wakati Malaika huyo alipokuja, akaelekeza mgongo Wake kwenye hema, kisha akamwulizia Sara, na kusema yale aliyosema jengoni. Ni wangapi wanaojua hilo? Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Lini? Kabla tu ya Sodoma kuteketezwa, hiyo ni kabla tu ya ulimwengu huu kuteketezwa. Ulimwengu wote usioamini utakuwa... utaingia katika machafuko, na kuteketea kwa moto mkali, tunajua hilo.

¹⁵⁷ Na kabla tu ya wakati huo, kumbukeni, ROHO MTAKATIFU ASEMA HIVI: Hii ndiyo ishara yenu ya mwisho. Liandike katika Biblia yako. Na kama jambo fulani likiinuka mbali na hili,

na kubwa kuliko hili, niiteni nabii wa uongo. Hilo ni tamshi kwelikweli. Mimi huangalia nisemayo. Ninawasiliana na zaidi ya watu milioni kumi kote ulimwenguni, mnaona, kwa hiyo sina budi kusema hivyo, nami ninajua sikusema hilo mimi mwenyewe.

¹⁵⁸ Sasa, Yeye yupo hapa. Siwezi kuwaponya, sina kitu cha kuwaponya nacho, bali Yeye ambaye amewaponya yupo hapa, akijaribu kuwafanya mwamini na kulikubali. Sasa, nawaomba, kama ndugu yangu, dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, aminini Ujumbe huu wa Injili.

¹⁵⁹ Na kama hamtaki kuniamini kwa sababu mimi si mfuasi wa dhehebu lenu, mimi si mfuasi wa dhehebu lolote. Mimi ni Mmethodisti, mimi ni—mimi ni Mpentekoste-Mmethodisti-Mnazarayo-Mpilgrim Holiness. Mnaona? Mimi ni ndugu yenu. Mimi ni Mmenoni-Muamishi, mimi ni—mimi—mimi ni hayo yote. Mnaona? Mimi—mimi—mimi ni ndugu yenu. Mnaona? Mimi ni Assembly, Church of God. Kila mmoja wenu ninyi ndugu wazuri ambao mmesaidia, watu wenu kote ulimwenguni wameidhamini mikutano yangu, na kukaa nyuma yangu katika nchi za kigeni, na kuniunga mkono, ndugu, niko papa hapa kuwakilisha, mimi ni ndugu yenu, ni—ninawatetea asilimia mia moja.

¹⁶⁰ Nina furaha kwa ajili yenu, usiku wa leo, katika saa hii kuu ya giza kujua ya kwamba ninyi ni wanaume na wanawake wa Mungu, mmekeki hapa kuwakilisha Injili hii kuu tunayohubiri. Msione aibu, ndugu, mnayo kweli, dumuni nayo. Msiiondokee, kulia wala kushoto, dumuni moja kwa moja nayo.

¹⁶¹ Ni wangapi huko nje, ambao hawana kadi za maombi, ambao ni wagonjwa? Hebu tukuone ukiinua mkono wako, popote ulipo. Kulikuwako na mwanamke katika Biblia, kama tulivyosema hivi majuzi usiku, asiyekuwa na kadi ya maombi, lakini akasema, “Ninaamini hadithi hiyo kuhusu Mtu huyo. Kama ninaweza kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima.” Ni wangapi wanaojua hadithi hiyo? Wakati alipomgusa, alitoka akaenda akaketi chini.

Naye Yesu akasema, “Ni nani aliyenigusa?”

Ndipo Petro akamkemea, akisema, “Kila mtu anakugusa.”

Akasema, “Lakini nimekuwa dhaifu.”

¹⁶² Ni wangapi wanaojua ya kwamba *nguvu* hizo zinamaanisha “uweza?” Dhaifu, akawa dhaifu. Hiyo ndiyo sababu huwezi kwenda. Hivi karibuni, hii hapa ikija tena, nitaondoka hudumani. Huduma yangu itabadilika, siwezi kuwa mwinjilisti na mwonaji kwa wakati ule ule, inawajenga watu chini ya tumaini la uongo. (Hiyo ni mara mbili.) Sasa... (Jamani, laiti hiyo isingefanya hivyo.)

¹⁶³ Lakini angalieni, sasa, katika kusanyiko hili, kwa ajili ya usiku wa leo, kama Mungu ataonyesha ishara moja kama hiyo,

ya kwamba Yeye yuko hapa pamoja nasi, ninyi nyote mtaamini kwa moyo wenu wote?

¹⁶⁴ Basi kama mwanamke huyo aligusa vazi Lake, na ndipo Yeye akageuka na kumwambia ya kwamba alikuwa anatokwa na damu, na kusema, Yeye kamwe hakusema, “Nilifanya hivyo *mimi*,” Yeye alisema, “*Imani yako* ilifanya hivyo,” (Hiyo ni kweli?) sasa, imani yako ndiyo itakayofanya jambo hilo. Hiyo ni kweli? Imani yako ndiyo inayofanya hivyo.

¹⁶⁵ Na hivi mmewaona makasisi wenu, wahudumu wenu, usiku wa leo? Kila usiku wanaketi hapa nyuma yangu, kuniombea, badala ya kuketi huko nje wakaitwe mstarini. Wengi wao tayari wameponywa, najua hilo. Wao ni wagonjwa, pia, wao ni wahitaji, bali wanapendelea kusanyiko lao kwanza, hao ni wachungaji. Sasa, ninyi aminini.

¹⁶⁶ Sasa, ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, usiku wa leo, ambaye alikuwa wakati huo? Yuko wapi? Ameketi mkono wa kuume wa Baba. Hiyo ni kweli? Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na nini? Mambo ya udhaifu wetu. Je, hiyo ni kweli? Anaweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Vema. Kama anaweza kuguswa, Naye ni Kuhani Mkuu yeye yule, angetendaje, usiku wa leo, kama ulingusa? Vile vile alivyofanya wakati huo. Hiyo ni kweli? Kila mtu anayeamini hilo, aseme . . . inua mkono wako, kote kote, kila mahali. Vema.

¹⁶⁷ Sasa, nitangojea tu kidogo, ninangojea kusanyiko litulie, liwe na kicho. Roho Mtakatifu ni mwoga *sana*. Loo, jambo moja tu dogo, Yeye ata—Yeye ataondoka, ataniacha tu, ndipo itanibidi kuondoka. Ninyi aminini.

¹⁶⁸ Sasa, ninyi watu, nasema, msio na kadi ya maombi, inueni mikono yenu. Nafikiri hakuna maombi. . . Sidhani aligawa kadi zozote za maombi, sivyo? Tutazigawa kesho, ama Jumapili, mojawapo, kwa ajili ya ibada ya Jumapili alasiri, ama kesho, wakati wowote Bwana atakapoongoza.

¹⁶⁹ Sasa, ninyi ombeni. Mnasema, “Ati Kuhani Mkuu?” Sio William Branham, la, William Branham ni mwanadamu, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema, kama tu ulivyo wewe. “Lakini, Bwana, ninaamini huyu mtu aliniambia kweli, ni Biblia. Ananiambia ya kwamba hii ndiyo siku ambayo Mungu aliahidi jambo hilo.”

¹⁷⁰ Sasa, ninawatakeni baadhi yenu watu ambao si walemavu, kwanza tutaninii, kisha tutawaendea walemavu baadaye. Sasa, kama ningaliangalia hapa, niseme, “Maskini msichana huyu, ni mlemavu,” Ningesema, “maskini mvulana huyu hapa mwenye gango hili mguuni mwake,” huenda nikakisia hilo, niseme, “labda alikuwa na polio, alifanya hivyo.” Loo, hakika, mtu yeyote anaweza kuangalia hilo, mnaona, “Mvulana huyu ni mlemavu, mwanamke huyu ni mlemavu,” hakika, mtu yeyote anaona hilo. Bila shaka. Huo usingekuwa ni muujiza. Lakini vipi

kuhusu wewe huko nje unayeonekana mzima na mwenye afya? Huyu ndiye, huyo ndiye. Ninyi ombeni.

¹⁷¹ Sasa, Baba yetu wa Mbinguni, hapa kuna lundo la leso zimewekwa hapa, nazo zinawawakilisha wagonjwa. Nao wanazileta hizi, kwa sababu kwamba katika Biblia walichukua kutoka kwenye mwili wa Paulo leso na nguo, na Biblia ilisema ya kwamba pepo wachafu waliwatoka, pepo waliwatoka, waliponywa. Watu hawa katika wakati mwingine wanaamini vivyo hivyo, kwa sababu walikuwa wamekuona Wewe ukitenda kazi ndani ya Paulo, walijua ya kwamba alikuwa mtumishi Wako. Naye Paulo ameondoka muda mrefu uliopita, Bwana, kwenda Utukufuni, bali Wewe ungali ni Roho Mtakatifu yeye yule aliyekuwa juu yake. Uliahidi ya kwamba ungefanya jambo lile lile, Nawe unalifanya.

¹⁷² Sasa, mwandishi mmoja alisema ya kwamba wakati Israeli walipokatiliwa mbali kutoka kwenye nchi ya ahadi, nayo Bahari ya Shamu ilikuwa inazuia, kwamba Mungu alichungulia chini kupitia ile Nguzo ya Moto kwa macho yenye hasira, na hiyo Bahari ya Shamu ikaogopa, nayo ikarudi nyuma, nao wana wa Israeli wakavuka wakaingia katika nchi ya ahadi. Sasa, Bwana, angalia usiku wa leo, kupitia Damu ya Yesu, na kila moja ya leso hizi, zinapowekwa juu ya watu, jalia huyo ibilisi aogope, na kurudi nyuma, jalia mgonjwa huyo aingie katika ahadi hiyo nzuri ya uponyaji wa Kiungu. Kama ulivyosema, “Zaidi ya mambo yote, naomba ufanikiwe katika afya.” Tujalie Bwana, katika Jina la Yesu Kristo, ninaomba. Amina.

¹⁷³ Sasa, tunapoketi, ninataka kila mtu kwa uchaji na utulivu, kicho kabisa, kuwa mtulivu, uwe tu katika maombi, na moyoni mwako useme, “Bwana Yesu, jalia niguse vazi Lako. Ninajua Ndugu Branham hanijui, hajui mimi ni nani, wala mahali nilipo, wala chochote kunihusu mimi. Lakini kama Wewe utageuza tu... Naye ananiambia ya kwamba tunasoma ambapo kwamba watu wanazaliwa ulimwenguni kwa ajili ya mambo fulani, kwa nyakati fulani, alisema tangu alipokuwa maskini mvulana mdogo... Tumesikia ya kwamba mambo haya yanakuja, ya kwamba... Kama utaniruhusu tu niguse vazi Lako, basi Wewe nena kupitia kwa Ndugu Branham, jalia aniambie kile ninachoombea, kile kilichonileta hapa, *kitu fulani*, nitakuamini Wewe.” Sema tu hilo. Sema, “Sina shaka Bwana, bali nina haja.” Iweni tu na imani na kuamini. Ninii tu, tunangojea, kwa unyenyekevu, kwa utamu, tuingojea, hakuna mtu anayesukuma sasa, iweni tu... jistarehesheni tu.

¹⁷⁴ Sasa, kama kila mtu anaweza kuona kile ninachooona, kama unataka kuangalia, kuna mtu aliyeketi moja kwa moja huko nyuma, kwanza kabisa ana ugonjwa wa moyo, jambo lingine, ana mgando wa damu kifuani mwake. Ninaamini ataukosa. Anatoka Michigan, Bw. Hannah, simama kwa miguu yako, bwana. Pokea uponyaji wako, Yesu Kristo anakuponya.

¹⁷⁵ Ukiwa umesimama kwa miguu yako, bwana, hivi mimi na wewe tunafahamiana, mmoja kwa mwingine? Inua mkono wako. Mambo hayo yaliyosemwa, kila kitu kilichosemwa kilikuwa ni kweli? Punga mkono wako namna *hii* kwa kusanyiko. Hivi si ulikuwa ukiomba Mungu akuguse, yule Kuhani Mkuu? Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako *hivi*. Umeponywa.

¹⁷⁶ Futi arobaini kutoka kwangu, aligusa nini? Aligusa nini? Je, hilo linaifanya Biblia kuwa kweli, ndugu? Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Unaamini hilo?

¹⁷⁷ Sasa, mtu mwingine, mahali fulani, omba. Ninaweza tu kusema ninapoitazama Nuru hiyo na kuhisi roho yako ikivuta. Si uteuzi wangu, ni wa Baba, ninazungumza tu. Lakini nisipozitenda kazi za Yesu Kristo, basi mimi si shahidi Wake. Si lazima nifanye hivyo, hiyo ndiyo huduma yangu; hawa watu si lazima wafanye hivyo, hawatafanya hivyo. Hakuna... Nami nitasema hivi, katika Jina la Bwana: Hakuajakwako, wala hakutakuwako, mpaka nitakapoondoka; kile hasa Yeye alichoniambia wakati alipoiagiza.

¹⁷⁸ Mtu aliyeketi papa hapa nyuma, ametiwa uvuli wa mauti, ndiyo kwanza afanyiwe upasuaji wa kansa, bali haukufaulu. Bw. Holtzinger, simama kwa miguu yako, na uamini. Hivi mimi ni mgeni kwako, bwana? Inua mkono wako. Je, mambo hayo ni kweli? Kila kitu ni kweli? Punga mkono wako namna *hii* kama hiyo ni kweli. Mwamini Bwana Yesu Kristo, nenda, uwe mzima. Amini kwa moyo wako wote.

¹⁷⁹ Kuna roho ya kansa mahali fulani, unaihisi tu, kivuli cha ibilisi. Sio mimi, sasa wewe acha kuwazia hilo, sio mimi, Yeye. Hapa, angalia moja kwa moja kule. Hivi huwezi kuiona hiyo Nuru, ndugu? Angalieni, imesimama pale pale. Mnaiona? Iko papo hapo juu ya mtu yule aliyeketi pale amevaa hiyo tai nyekundu. Mtu huyo ana lukemia. Hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako, bwana. Kama ulikuwa umeketi hapo ukiuombea huo, simama kwa miguu yako, kama mambo hayo ni... ni kweli. Je, tunafahamiana? Punga mkono wako huku na huku. Mambo uliyoambiwa, ni ya kweli? Punga mkono wako tena. Mwamini Bwana Yesu Kristo, na uponywe. Unaona?

¹⁸⁰ Angalieni, angalieni hapa, mnamwona mama huyu aliyeketi papa hapa? Unamwombea mtoto huyo mchanga. Mtoto mchanga hawezi kuishi duniani nje ya Mungu. Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, mtumishi Wake? Kama nikikwambia mtoto huyo ana shida gani, utaamini atapona? kama unawasiliana vya kutosha kuamini. Huyu mtoto mchanga ana shimo kwenye moyo wake. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, Dada. Unaamini sasa? Weka mkono wako juu yake, jinsi tu ulivyofanya.

¹⁸¹ Mungu, ninamkemea ibilisi huyo. Jalia mtoto huyo mchanga aishi, katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁸² Hapa, mwanamke huyu alikuwa mgonjwa sana, mama huyu aliyelala hapa. Angalia huku, Dada, papa hapa. Unaonekana kuwa ndiye mgonjwa kuliko wote wa kundi hili. Ulikuwa unaomba. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, mtumishi Wake?

¹⁸³ Niliona kiti cha magurudumu, mahali fulani, kikijitokeza. Ni yule mtu aliyeketi pale pale, amekuwa na kiharusi. Yeye ni mhubiri, jina lake ni Bw. Fergusson. Mwamini Bwana Yesu Kristo, utatoka kwenye hicho kiti. Mimi siwaponyi watu.

¹⁸⁴ Samahani, mama, ilinibidi kuifuata, niliona wewe ni mgonjwa sana. Bila shaka. Dada yako hapa, anayekuangalia, anakupenda. Umetiwa uvuli wa mauti, unajua hilo. Huwezi kuishi nje ya Mungu, akina Mayo wanajua hilo, sivyo? Umetoka kwa Mayo, umekuwa kwa Mayo huko juu, Kliniki ya Mayo. Kansa inakuua. Walikuleta hapa chini kwa ajili ya mkutano huu, hiyo ni kweli. Dada yako anaweza kushuhudia hilo.

¹⁸⁵ Siwezi kukuponya, lakini hebu nikuulize jambo fulani. Kulikuwa na wenye ukoma watatu, wakati mmoja, walioketi langoni wakati Samaria ilipokuwa imezingirwa na Washami, wakasema, "Kwa nini tuketi hapa mpaka tufe? Kama tukikaa hapa, hakika tutakufa, tukiingia mjini tutakufa kwa vyovyote vile, maana wanakula watoto wao kwa wao mle ndani." Lakini kasema, "Vipi kama tukishuka kwenda kwenye kambi ya adui? Wakituu, tutakufa tu kwa vyovyote vile, bali kama tukinini—kama tukiokolewa tukiwa hai, tutaishi." Mungu aliheshimu hilo, sivyo? Nao waliokolewa, kisha wakauokoa um-...

¹⁸⁶ Umeketi mahali pale pale. Mayo walikukatia tamaa, Bibi Mason. Ajabu nilikujua, kwamba wewe ni nani. Sasa, lakini nataka kuuliza...Walikukatia tamaa, hakuna kitu wanachoweza kukufanyia. Ukilala hapa utakufa, ukienda kwa Mayo, utakufa, huombwi kwenda kwenye nyumba ya adui, unatazamia kuwa...kuja katika nyumba ya Baba, usiku wa leo, apate kukuponya. Unaamini kwa moyo wako wote? Ningesimama, na kuchukua machela hiyo, na kuondoka hapa, na kwenda nyumbani, niponywe.

¹⁸⁷ Vipi kukuhusu wewe, mama huko kwenye hiyo machela, unayeangalia huku, unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Naam. Unaamini kwa ninii yako yote...? Maskini uvimbe huo kwenye koloni na kadhalika utakuacha. Unaamini? Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Basi simama utoke hapo, katika Jina la Yesu Kristo. Simama kwa miguu yako!

Huyo hapo, mlemavu...?...Mnaamini? Kila mtu anaamini kwa moyo wako wote?

¹⁸⁸ Njoni hapa, ndugu. Shukeni, mkaweke mikono yenu juu ya wagonjwa na wanaoteseka. Shukeni pale. Shukeni, mkaweke mikono yenu juu ya...?...

¹⁸⁹ Ninataka kuwaulizeni: Je, hizo ni kazi za Yesu Kristo? Inueni mikono yenu, na kusema, “Amina.” Hawa hapa watumishi wa Mungu wanakuja kuweka mikono ninapoomba.

¹⁹⁰ Hebu... Kila mmoja wenu kwenye viti vya magurudumu, haidhuru uko wapi, hii ndiyo saa yako, huu ndio wakati wa uponyaji wako. Nitaomba. Hebu kusanyiko lisimame, simameni kwa miguu yenu, sijali wewe ni nani.

¹⁹¹ Kila mmoja wenu ninyi watu wa Mungu shukeni huko chini, na kuwawekea watu hawa mikono. Nitawaombea huku mkiweka mikono yenu juu yao. Na kila...

¹⁹² Angalieni vile viti vya magurudumu na vitanda vya wagonjwa, wakisimama! Wekeni mikono yenu juu yao, ndugu.

¹⁹³ Mwenyezi Mungu, uliyemfufua Yesu Kristo katika wafu, na umeshinda kila adui, juu ya ibilisi, ninampa changamoto kila ibilisi: Toka ndani ya watu hawa, katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁹⁴ Waache, Shetani, wameponywa. Kristo...?... 

61-0414 Msiogope, Ni Mimi
Illinois Wesleyan University
Bloomington, Illinois Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org